SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR

WIZARA YA ARDHI NA MAENDELEO YA MAKAAZI

HOTUBA YA WAZIRI WA ARDHI NA MAENDELEO YA MAKAAZI

MHESHIMIWA RAHMA KASSIM ALI (MBM)

KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2023/2024

JUNI, 2023

YALIYOMO

UTANGULIZI 1
UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA WIZARA YA ARDHI NA MAENDEELO YA MAKAAZI KWA MWAKA WA FEDHA 2022 - 2023. 5
MAPATO NA MATUMIZI 5
TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA KAZI KWA PROGRAMU ZA WIZARA KWA MWAKA WA FEDHA 2022/2023. 7
PROGRAMU KUU PN0201: UENDESHAJI NA URATIBU WA WIZARA YA ARDHI NA MAENDELEO YA MAKAAZI 7
PROGRAMU NDOGO YA URATIBU WA MIPANGO, SERA NA UTAFITI 7
PROGRAMU NDOGO YA UENDESHAJI NA UTUMISHI. 12
PROGRAMU NDOGO YA URATIBU WA SHUGHULI ZA WIZARA PEMBA 14
PROGRAMU KUU PN0202: USIMAMIZI WA ARDHI 16
PROGRAMU NDOGO YA USIMAMIZI WA ARDHI 16
PROGRAMU KUU PN0203: MAENDELEO YA MAKAAZI 24
PROGRAMU NDOGO YA MAENDELEO YA MAKAAZI 24
TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA SHIRIKA LA NYUMBA ZANZIBAR 31
CHANGAMOTO NA HATUA ZA UTATUZI WAKE 34
MWELEKEO WA MAKADIRIO YA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2023/2024 36
VIPAOMBELE VIKUU VYA WIZARA KWA MWAKA WA FEDHA 2023/2024 36
PROGRAMU KUU PN0201: UENDESHAJI NA URATIBU

WA WIZARA YA ARDHI NA MAENDELEO YA MAKAAZI 38
PROGRAMU NDOGO YA URATIBU WA MIPANGO, SERA NA UTAFITI 39
PROGRAMU NDOGO YA UTAWALA NA UENDESHAJI 40
PROGRAMU NDOGO YA URATIBU WA SHUGHULI ZA WIZARA PEMBA 41
PROGRAMU KUU PN0202: USIMAMIZI WA ARDHI 42
PROGRAMU NDOGO YA USIMAMIZI WA ARDHI 43
PROGRAMU KUU PN0203:MAENDELEO YA MAKAAZI 47
PROGRAMU NDOGO YA MAENDELEO YA MAKAAZI 48
MUWELEKEO WA BAJETI YA SHIRIKA LA NYUMBA ZANZIBAR 52
SHUKURANI 54
MAOMBI YA FEDHA KWA MWAKA 2023/2024 56
HITIMISHO 57
VIAMBATISHO 58

HOTUBA YA WAZIRI WA ARDHI NA MAENDELEO YA MAKAAZI MHESHIMIWA RAHMA KASSIM ALI (MBM) KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2023/2024 KATIKA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

UTANGULIZI

1. **Mheshimiwa Spika,** kwa ruhusa yako, naomba kuwasilisha Hotuba ya bajeti ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya kazi za Kawaida na Maendeleo kwa mwaka wa fedha 2023/2024 kwa Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi.

2. **Mheshimiwa Spika,** awali ya yote, naomba nichukuwe nafasi hii adhimu kumshukuru Mwenyezi Mungu (S.W) Mwingi wa Rehema kwa kutujaalia afya njema, uwezo na nguvu za kutekeleza yale yote tuliyojipangia katika kuwatumikia wananchi wa Zanzibar. Vile vile, kwa rehema za Mwenyezi Mungu Mtukufu ametuwezesha kukutana hapa leo tukiwa katika hali ya usalama, amani na utulivu katika uwasilishaji wa hotuba ya bajeti ya Wizara hii mbele ya Baraza lako.

3. **Mheshimiwa Spika,** kwa niaba ya Viongozi na Wafanyakazi wote wa Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi, napenda kuchukua fursa hii kumpongeza kwa dhati kabisa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt Samia Suluhu Hassan kwa kazi nzuri iliyotukuka

anayoifanya katika kuwaletea Maendeleo Wananchi wa Tanzania kwa ujumla kwa kuzingatia misingi ya haki na uwajibikaji pamoja na kusimamia na kutekeleza vyema Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya Mwaka 2020 – 2025, kwani ni wazi kuwa Mheshimiwa Rais anatekeleza Ilani ya Chama kwa vitendo katika kupeleka maendeleo kila pembe ya Tanzania, naomba Mwenyezi Mungu azidi kumsimamia katika kuendelea kutekeleza majukumu yake.

4. **Mheshimiwa Spika,** kwa namna pekee naomba kuchukuwa fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Hussein Ali Mwinyi kwa namna anavyoingoza nchi yetu na kuhakikisha anawaletea maendeleo wananchi wake. Pia nampongeza tena kwa ufuatiliaji makini wa utendaji wa Serikali anayoiongoza, pamoja na miongozo anayotupatia katika kuhakikisha kwamba Wizara na Taasisi zote zinatoa huduma bora kwa wananchi na kwa wakati muafaka. Naomba Mwenyezi Mungu amzidishie nguvu, afya, hekima na busara katika uongozi wake na kuweza kufikia azma yake ya kuiletea maendeleo makubwa nchi yetu.

5. **Mheshimiwa Spika,** natoa shukrani zangu za dhati na kuwapongeza Makamo wa Kwanza wa Rais Mheshimiwa Othman Masoud Othman na Makamo wa Pili wa Rais Mheshimiwa Hemed Suleiman Abdulla kwa jitihada wanazozichukua katika kumsaidia Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. Jitihada hizo ni pamoja na ufuatiliaji wa kazi zinazotekelezwa na Serikali na uhamasishaji wa amani, umoja na mshikamano

katika nchi yetu. Allah azidi kuwapa nguvu, busara, hekima, na afya njema ili waweze kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi zaidi.

6. **Mheshimiwa Spika,** kwa namna ya pekee, napenda kukupongeza wewe binafsi pamoja na Naibu Spika na wasaidizi wako kwa busara na hekima mnazozitumia katika kuliongoza Baraza hili. Aidha, naomba kuwashukuru wajumbe wa Kamati ya Mawasiliano, Ardhi na Nishati ya Baraza la Wawakilishi ikiongozwa na Mwenyekiti wake Mheshimiwa Yahya Rashid Abdallah pamoja na Kamati nyengine za Baraza la Wawakilishi kwa ushirikiano wao, ushauri na maelekezo mbali mbali ambayo wamekuwa wakitupatia katika kufanikisha utekelezaji wa majukumu ya Wizara hii.

7. **Mheshimiwa Spika,** naomba pia kutoa shukrani za pekee kwa Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makaazi Mheshimiwa Juma Makungu Juma kwa ushirikiano wake mkubwa anaonipa katika kuiongoza Wizara hii. Aidha, napenda kutoa shukrani zangu kwa Katibu Mkuu Dkt Mngereza Mzee Miraji, Naibu Katibu Mkuu, ndugu, Mzee Ali Haji, Afisa Mdhamini ndugu, Bakari Ali Bakari Wakurugenzi wa Mipango na Utumishi, Wakuu wa Taasisi pamoja na Watendaji na wafanyakazi wote wa Wizara hii ambao kwa pamoja wanaendelea kunipatia ushirikiano wao wa hali ya juu katika kuongoza na kutekeleza majukumu ya Wizara na kuhakikisha kwamba wananchi wa Zanzibar wanafaidika na huduma zinazotolewa na Wizara hii.

8. **Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi kimuundo inajumuisha Idara na Taasisi zifuatazo:-

   i. Idara ya Mipango Sera na Utafiti,

   ii. Idara ya Uendeshaji na Utumishi,

   iii. Ofisi Kuu Pemba,

   iv. Kamisheni ya Ardhi (COLA)

   v. Mahakama ya Ardhi,

   vi. Ofisi ya Mthamini Mkuu wa Serikali,

   vii. Wakala wa Majengo Zanzibar (ZBA) na

   viii. Shirika la Nyumba Zanzibar (ZHC)

9. **Mheshimiwa Spika,** Aidha, Wizara inazo Bodi Tendaji (Executive Boards) Nne (4) ambazo ni:-

   i. Bodi ya Kudhibiti Kodi za Nyumba,

   ii. Bodi ya Kondominio,

   iii. Bodi ya Usajili wa Wakandarasi na

   iv. Bodi ya Usajili wa Wahandisi, Wasanifu na Wakadiriaji Majengo.

10. **Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi inatekeleza majukumu yake ya msingi yafuatayo: -

    a. Kutunga na kusimamia utekelezaji wa Sera za kisekta na Sheria zinazohusiana na Ardhi, Nyumba na Makaazi;

b. Kushajihisha na kutekeleza upatikanaji wa makaazi bora na nafuu kwa wananchi na viongozi;

c. Kufanya tafiti zinazohusiana na Sekta ya Ardhi, Nyumba na Makaazi;

d. Kutayarisha na kusimamia utekelezaji wa Mipango ya matumizi bora ya ardhi Mijini na Vijijini;

e. Kusimamia utambuzi, usajili na umiliki wa ardhi;

f. Kusimamia shughuli za ujenzi ikiwemo usanifu wa majengo na Wakandarasi;

g. Kusimamia Rasilimali watu, fedha na rasilimali nyenginezo za Wizara.

11. Mheshimiwa Spika, baada ya utangulizi huo naomba sasa uniruhusu kuelezea utekelezaji wa kazi za kawaida na za maendeleo za Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi kwa kipindi cha Mwaka wa Fedha 2022/2023 pamoja na muelekeo wa Makadirio ya Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024.

UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA WIZARA YA ARDHI NA MAENDEELO YA MAKAAZI KWA MWAKA WA FEDHA 2022 - 2023.

MAPATO NA MATUMIZI

12. Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha 2022/2023 Wizara yangu ilipangiwa kukusanya jumla ya **TZS Bilioni 2.922** kutoka vyanzo vya Wizara, ambapo **TZS Bilioni 1.900** kutoka katika vianzio vilivyomo ndani ya fungu la Wizara,

na **TZS Bilioni 1.022** kwa ajili ya Mapato yanayotokana na vianzio mbali mbali vilivyomo ndani ya Fungu la Kamisheni ya Ardhi. Hadi kufikia Machi, 2023 jumla ya **TZS Bilioni 2.6** zimekusanywa. Kiwango hichi ni sawa na asilimia **89** ya makadirio ya Mwaka na **asilimia 106** kwa ulinganisho ya makadirio ya makusanyo ya miezi tisa. Kwa ufafanuzi zaidi naomba angalia **Kiambatisho "B1"**

13. **Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023, Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi ilipangiwa kutumia Jumla ya **TZS Bilioni 26. 942** kati ya hizo **TZS Bilioni 5.725** ni kwa ajili ya utekelezaji wa kazi za kawaida kwa fungu la Wizara, ambapo kati ya fedha hizo jumla ya **TZS Bilioni 2.558** zilitengwa kwa ajili ya mishahara kwa Idara zilizo chini ya Wizara, **TZS Bilioni 1.183** kwa ajili ya matumizi ya kawaida ya uendeshaji wa ofisi kwa Idara zilizo chini ya Wizara na **TZS Bilioni 1.984** ni ruzuku kwa ajili ya Taasisi za Wizara na **TZS Billioni 17.0** kwa ajili ya kazi za Maendeleo. Vilevile Jumla ya **TZS Bilioni 4.216** zilitengwa kwa kazi za kawaida, ruzuku na mishahara kwa ajili ya fungu la Kamisheni ya Ardhi.

14. **Mheshimiwa Spika,** Hadi kufikia Machi, 2023 Jumla ya **TZS Bilioni 6.6** zimepatikana ambapo **TZS Bilioni 4.97** kwa ajili ya Mishahara sawa na **asilimia 114** ya makadirio, **TZS Bilioni 1.67** kwa ajili ya matumizi ya kawaida sawa na **asilimia 30** ya makadirio ya fedha zilizopangwa na kwa upande wa Miradi ya Maendeleo hakuna fedha iliyopatikana. Kwa ufafanuzi zaidi naomba angalia **Kiambatisho "C1"**

TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA KAZI KWA PROGRAMU ZA WIZARA KWA MWAKA WA FEDHA 2022/2023.

15. **Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa utekelezaji wa shughuli za Wizara, kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023 Wizara ilifanikiwa kutekeleza majukumu yake kupitia Programu kuu tatu zifuatazo:-

a. Programu PN0201: Uendeshaji na Uratibu wa Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi

b. Programu PN0202: Usimamizi wa Ardhi.

c. Programu PN0203: Maendeleo ya Makaazi.

PROGRAMU KUU PN0201: UENDESHAJI NA URATIBU WA WIZARA YA ARDHI NA MAENDELEO YA MAKAAZI

16. **Mheshimiwa Spika,** Programu hii ina jukumu la kuimarisha uratibu katika utekelezaji wa kazi za Wizara ambayo inajumuisha programu ndogo tatu ambazo zinatekelezwa na Idara ya Mipango, Sera na Utafiti, Idara ya Uendeshaji na Utumishi na Afisi Kuu Pemba. Kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023 utekelezaji wa programu hii ni kama ifuatavyo: -

PROGRAMU NDOGO YA URATIBU WA MIPANGO, SERA NA UTAFITI

17. **Mheshimiwa Spika,** Idara ya Mipango Sera na Utafiti inajukumu la kuratibu na kusimamia utayarishaji wa

Mipango ya Taasisi zote zilizomo ndani ya Wizara ikiwemo Sera, Sheria na Bajeti. Katika Mwaka wa Fedha 2022/2023 Programu hii ndogo ililenga kutekeleza shughuli za uratibu na uandaaji wa Mipango na Miongozo ya Kisera ya utekelezaji wa kazi za Wizara, kuratibu uandaaji wa mapitio ya sheria, kusimamia na kufuatilia utekelezaji wa shughuli na Miradi ya Maendeleo, kuendeleza tafiti kwa ajili ya kuimarisha utoaji wa huduma pamoja na kuratibu vikao mbalimbali vya mashirikiano baina ya SMT na SMZ.

18. **Mheshimiwa Spika,** hadi kufikia mwezi wa Machi, 2023 Idara ya Mipango, Sera na Utafiti imefanikiwa kutekeleza kazi zifuatazo:-

i. Kuratibu na kuandaa Mipango ya Wizara

19. **Mheshimiwa Spika,** Idara imeratibu vikao vya majadiliano na Kampuni mbalimbali ambazo zimeonesha nia ya kuwekeza katika miradi ya ujenzi wa nyumba za makaazi ya bei nafuu kwa wananchi, nyumba za biashara pamoja na usimamizi wa ardhi. Miongoni mwa Kampuni hizo ni Aser Construction and Technology Limited, IGNFI, na SINOTEC Company limited ambapo Kampuni ya Aser Construction and Technology Limited, Kampuni ya SINOTEC na IGNFI, tayari Wizara imeshatiliana Saini Hati za Makubaliano (MoU) kwa ajili ya utekelezaji wa miradi hiyo.

ii. Kuratibu na kusimamia mapitio ya Sheria na Sera za Wizara.

20. **Mheshimiwa Spika,** katika kuandaa miongozo ya Kisera na Kisheria, Idara ya Mipango, Sera na Utafiti kwa kushirikiana na Tume ya Kurekebisha Sheria pamoja na

Taasisi zote za Wizara, inaendelea kufanya mapitio ya Sheria zinazosimamia Sekta ya Ardhi ili ziweze kuleta ufanisi zaidi na kuendana na mabadiliko yanayojitokeza. Wizara tayari imeshakamilisha mapitio ya Sheria ya Mthamini Mkuu wa Serikali, Sheria ya kudhibiti Kodi za Nyumba na Sheria ya Mahakama ya Ardhi na tayari zimeshawasilishwa katika Sekretarieti ya Kamati ya Makatibu Wakuu kwa hatua stahiki. Vilevile Sheria ya Mipango Miji na Vijiji nayo ipo katika hatua ya kuwasilishwa kwenye kikao cha Kamati ya Uongozi ya Wizara.

Aidha, katika kuhakikisha Zanzibar inakua na Miji iliyopangwa vizuri, Idara inaendelea kuratibu utayarishaji wa Sera ya Makaazi pamoja na Sera ya Mipango Miji na Vijiji ambapo Timu ya Wataalamu inaendelea na zoezi la uwasilishaji wa Rasimu ya Sera ya hizo kwa wadau mbalimbali, kwa ajili ya kupata maoni yao kwa lengo la kuziimarisha Sera hizo.

iii. Ufuatiliaji wa utekelezaji wa Mipango ya Sekta

21. **Mheshimiwa Spika,** Idara inaendelea na jukumu la kufuatilia na kutathmini utekelezaji (Monitoring and Evaluation) kwa kazi za Wizara. Lengo la zoezi hili ni kuhakikisha kwamba mipango ya Wizara inatekelezwa kwa ufanisi na kufikia malengo yaliyokusudiwa kwa kuzingatia matumizi sahihi ya fedha na wakati. Miongoni mwa kazi zilizofuatiliwa ni Migogoro ya ardhi ambayo imejitokeza katika maeneo mbalimbali Unguja na Pemba na baadhi ya migogoro hiyo kupatiwa suluhisho. ***Kiambatisho F1 kinaonesha maoneo mbalimbali yenye migogoro ya ardhi iliyofuatiliwa.***

22. **Mheshimiwa Spika,** Vilevile Idara imefanya ufuatiliaji wa mradi wa matengenezo ya nyumba ya maendeleo Michenzani (bloki namb.1) ngazi ya ya tatu, maeneo ya uwekezaji ambapo yanatarajiwa kuwepo kwa miradi ya maendeleo kama vile Kisakasaka, Tunguu na Dunga. Katika kuhakikisha miradi ambayo Wizara imepanga kutekeleza kwa usahihi, Idara imefanya Tathimini ya matengenezo ya nyumba za Maendeleo Unguja na Pemba kwa ajili ya kutekeleza Mradi wa ukarabati wa nyumba za Maendeleo. Tathmini hiyo imewezesha kuandaliwa kwa "Bill of Quantity" (BOQ), Michoro na kutambua mahitaji halisi yanayohitajika katika ukarabati huo.

iv. Kuratibu mashirikiano baina ya Wizara za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar (SMZ) na Serikali ya Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania (SMT).

23. **Mheshimiwa Spika,** katika kutekeleza muongozo uliotolewa na Ofisi ya Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar ambao umeziagiza Wizara zinazoshabihiana kimajukumu, kukutana na kubadilishana uzoefu na utaalamu. Idara ya Mipango imeratibu na kushiriki kikao cha Ushirikiano baina ya Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi (SMZ) na Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi (Sekta ya Ujenzi SMT) na Wizara ya Ujenzi Mawasiliano na Uchukuzi (SMZ) ngazi ya Makatibu Wakuu na Mawaziri ambacho kimefanyika tarehe 13 – 17 Novemba, 2022, Zanzibar. Kikao hicho kiliwezesha Wizara kutiliana saini Hati ya Makubaliono na Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi SMT kuhusu ushirikiano wa kiutendaji baina ya Bodi za

ujenzi. Jambo ambalo litawezesha Bodi pacha kufanya kazi kwa mashirikiano ya karibu na kila upande kufaidika na mashirikiano hayo.

24. **Mheshimiwa Spika,** Vilevile Idara iliratibu kikao cha ushirikiano baina Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi (SMZ) na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makaazi (SMT) ambavyo vilifanyika Zanzibar tarehe 5 hadi 6 Disemba 2022 ngazi ya Wataalamu na tarehe 13 Januari 2023, ngazi ya Makatibu Wakuu. Vikao hivyo viliwezesha kuandaliwa kwa Hati ya Makubaliano baina ya Wizara mbili kwa lengo la kurahisha utendaji kazi na kubadilishana uzoefu baina ya Wizara na Taasisi kutoka SMT na SMZ.

25. **Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi kupitia Idara ya Mipango iliweza kushiriki Vikao vya Wadau vya maandalizi ya ushirikiano kati ya Tanzania na India (JPC) ambapo maeneo ya ushirikiano kati ya India na Tanzania katika Sekta ya Ardhi na Makaazi kwa Zanzibar na Tanzania Bara yaliwasilishwa. Pia, Idara ilishiriki kikao cha maandalizi ya maadhimisho ya Ushirikiano wa Kidiplomasia kati ya Tanzania na China ambayo yanatarajia kufanyika mwaka 2024.

26. **Mheshimiwa Spika,** Kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2022/23 jumla ya **TZS Milioni 918** zilipangwa kukusanywa kutokana na Ada za Vibali vya Ujenzi. Hadi kufikia Machi 2023, fedha zilizokusanywa ni **TZS Milioni 381.533** sawa **asilimia 42** ya makadirio.

27. **Mheshimiwa Spika,** katika Mwaka wa Fedha 2022/2023, jumla ya **TZS Milioni 335.270** ziliidhinishwa kutumika kwa utekelezaji wa Programu ndogo ya Uratibu wa Mipango, Sera na Utafiti. Hadi kufikia Machi, 2023 fedha zilizopatikana ni **TZS Milioni 194.148** ambapo **TZS Milioni 123.367** kwa ajili ya mishahara sawa na **asilimia 82** ya makadirio na **TZS Milioni 70.78** kwa ajili ya matumizi ya kawaida sawa na **asilimia 38** ya makadirio ya fedha zilizopangwa.

PROGRAMU NDOGO YA UENDESHAJI NA UTUMISHI.

28. **Mheshimiwa Spika,** lengo la Programu hii ni kusimamia uendeshaji wa shughuli za kila siku za Wizara pamoja na usimamizi wa rasilimali watu kwa kuandaa mipango ya kuwajengea uwezo Watumishi, kuimarisha mazingira bora ya kazi, kushughulikia haki na stahiki za Watumishi, kuhakikisha kuwepo kwa watendaji wa kutosha na wenye sifa pamoja na kusimamia nidhamu kwa watumishi wote wa Wizara na Taasisi zake.

29. **Mheshimiwa Spika,** katika kutekeleza majukumu yake ya msingi Idara ya Uendeshaji na Utumishi hadi kufikia Machi, 2023 imetekeleza kazi zifuatazo:-

    i. Kulipa stahiki kwa Wafanyakazi Ishirini na nane (28) ambao wamepatiwa posho za likizo, Wafanyakazi kumi na nne (14) wamelipwa posho za muda wa baada ya saa za kazi (Overtime), pamoja na kuratibu upatikanaji wa Stahiki kwa mfanyakazi mmoja (1) ambae alistaafu baada ya kumaliza muda wake wa utumishi.

ii. Kuratibu nafasi za ajira, ambapo jumla ya nafasi thalathini (30) ziliratibiwa katika fani mbali mbali zikiwemo fani za Uhandisi umeme, ujenzi, kompyuta na Wathamini ili kujaza nafasi tupu na nafasi mpya ambazo zilistahiki kupata waajiriwa wapya. Aidha, katika nafasi hizo ziliajiriwa nafasi kumi na tano (15), ambapo kupatikana kwake kumesaidia kupunguza pengo la watendaji wa fani mbali mbali zinazohitajika katika utekelezaji wa shughuli za kila siku za Wizara.

iii. Kuwapatia wafanyakazi saba (7) mafunzo ya muda mrefu na wafanyakazi nane (8) mafunzo ya muda mfupi. Aidha, Idara imewapatia mafunzo ya ndani ya sehemu ya kazi (on job training) wafanyakazi mia moja na sitini na nane (168) yanayohusiana na utunzaji siri na nyaraka pamoja na elimu kuhusu masuala ya rushwa wakati wa utekelezaji majukumu yao ya kila siku.

iv. Kutengeneza taarifa za Viongozi “Hard News Stories” thamanini (80), Matangazo “Social Media Stories” kumi na tano (15) na “Documenary tatu (3) kwa lengo la kuitambulisha Wizara juu ya utekelelezaji wa majukumu yake kwa jamii.

v. Katika kuhakikisha shughuli za Wizara zinatekelezeka kwa ubora na ufanisi Idara imesimamia huduma za kiofisi kwa asilimia 85% ikiwemo malipo ya umeme, vifaa vya kuandikia, ulinzi, usafi na upatikanaji wa maji.

vi. Kusimamia masuala ya usafiri kwa kazi za ofisi kwa kufanya matengenezo ya kawaida ya gari sita (6) na kuvifanyia “services” vyombo vinne (4) vya Wizara ,

pamoja na ununuzi wa mafuta ya petroli lita 6,225 na diseli lita 2,600 kwa ajili ya vipando vya Wizara.

30. **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2022/2023, Programu hii iliidhinishiwa jumla ya **TZS Bilioni 2.074** kwa ajili ya kufanikisha shughuli za uendeshaji na mishahara. Hadi kufikia Machi, 2023 fedha zilizopatikana ni **TZS Bilioni 2.068** ambapo **TZS Bilioni 1.9** kwa ajili ya mishahara sawa na **asilimia 118** ya makadirio na **TZS Milioni 207.7** kwa ajili ya matumizi ya kawaida sawa na **asilimia 42** ya makadirio ya fedha zilizopangwa.

PROGRAMU NDOGO YA URATIBU WA SHUGHULI ZA WIZARA PEMBA

31. **Mheshimiwa Spika,** programu hii ndogo inatekelezwa na Afisi Kuu Pemba ambayo inajukumu la kuratibu na kusimamia Utawala na Mipango ya kazi za Wizara zinazotekelezwa Pemba ikiwemo Programu na Miradi ya Maendeleo.

32. **Mheshimiwa Spika,** Hadi kufikia Machi, 2023 programu hii ndogo imetekeleza kazi zifuatazo: -

    i. Kulipa stahiki za wafanyakazi ambapo jumla ya wafanyakazi ishirini na nne (24) wamepatiwa malipo ya muda baada ya saa za kazi (overtime), malipo ya safari za kikazi kwa wafanyakazi (25), mafunzo ya muda mrefu kwa wafanyakazi (03) na muda mfupi kwa wafanyakazi (27) kati ya hao wanaume 11 na wanawake 16 juu ya kutumia mfumo wa E- Office. na wafanyakazi 03 kushiriki mafunzo juu ya uaandaaji wa

bajeti, andiko la dhana ya Mradi pamoja na upembuzi yakinifu kwa miradi mbalimbali.

ii. Kusimamia na kuratibu shughuli za kila siku za uendeshaji wa Afisi kwa kulipia gharama za malipo ya huduma za umeme, maji, simu, vifaa vya kuandikia, vifaa vya usafi, petroli, dizeli, gharama za posta pamoja na kufanya matengezo ya vyombo vya usafiri.

iii. Kufuatilia utekelezaji wa miradi ya maendeleo na shughuli mbalimbali zinazotekelezwa na Wizara kwa upande wa Pemba kama ifuatavyo:-

a. Eneo lililopangwa kwa ajili ya ujenzi wa Mji mpya wa Serikali Gomish Shehia ya Tibirinzi Chake Chake,

b. Maeneo ya ulipaji fidia kwa walioathirika na ujenzi wa barabara Meli Tano – Wete,

c. Ukaguzi wa eneo Mkoani –Ng'ombeni lililokua likitumiwa na Ofisi ya Shirika la Nyumba,

d. Eneo la ujenzi wa nyumba za Viongozi Pagali na Ofisi za Wakuu wa Mikoa na Wilaya (Chake, Mkoani, Wete na Micheweni),

e. Ujenzi wa Bustani ya Mwanamashungi Chake Chake,

f. Ukaguzi wa Nyumba za Maendeleo Mtemani na Micheweni pamoja na Ofisi ya Shirika la Nyumba Micheweni

g. Ukarabati wa Jengo la Posta lililopo Madungu Chake Chake.

33. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2022/2023 Afisi Kuu Pemba imepangiwa kukusanya jumla ya **TZS Milioni 97.00** Hadi kufikia Machi 2023 jumla ya **TZS Milioni 14.104** zimekusanywa sawa na **asilimia 14.5** ya makadirio.

    Kwa upande wa matumizi Afisi Kuu Pemba ilipangiwa kutumia jumla ya **TZS Milioni 747.600** kati ya fedha hizo **TZS Milioni 180.000** ni kwa ajili ya matumizi ya kazi za kawaida (OC) na **TZS Milioni 567. 600** ni kwa ajili ya malipo ya mishahara ya wafanyakazi. Hadi kufikia mwezi Machi 2023 fedha zilizopatikana ni jumla ya **TZS Milioni 658.410** ambapo **TZS Milioni 586.96** kwa ajili ya mishahara sawa na **asilimia 104** ya makadirio na **TZS Milioni 71.4** sawa na **asilimia 39** kwa ajili ya matumizi ya kawaida ya fedha zilizopangwa.

PROGRAMU KUU PN0202: USIMAMIZI WA ARDHI

34. **Mheshimiwa Spika,** Programu hii ina jukumu la kuhakikisha usalama wa matumizi ya ardhi na umiliki (Security of Land Tenure) kwa Wananchi na imegawika katika Programu ndogo kama ifuatavyo:-

PROGRAMU NDOGO YA USIMAMIZI WA ARDHI

35. **Mheshimiwa Spika,** katika Mwaka wa Fedha 2022/2023, jumla ya **TZS Bilioni 1.746** ziliidhinishwa kutumika kwa utekelezaji wa Programu ya Usimamizi wa ardhi kwa kazi za kawaida, maendeleo na mishahara. Hadi kufikia Machi, 2023 fedha zilizopatikana ni **TZS Milioni 333.381** sawa na **asilimia 23** ya makadirio, kwa upande wa kazi za maendeleo hakuna fedha iliyopatikana.

36. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2022/2023 Programu hii ililenga kutekeleza shughuli zote zinazohusiana na masuala ya Ardhi. Programu hii ndogo inatekelezwa na Taasisi zifuatazo: -

MAHAKAMA YA ARDHI

37. Mheshimiwa Spika, Mahakama ya Ardhi imeanzishwa chini ya Sheria Namba 7 ya Mwaka 1994. Lengo la kuanzishwa kwake ni kupokea, kusikiliza na kuyatolea uamuzi mashauri yanayotokana na migogoro ya ardhi yanayowasilishwa na wananchi.

38. Mheshimiwa Spika, hadi kufikia Machi, 2023 Mahakama ya Ardhi imetekeleza kazi zifuatazo:-

i. **Kuendelea kupokea, kusikiliza na kutoa uamuzi wa mashauri yanayohusiana na Migogoro ya ardhi iliyowasilishwa Mahakamani.**

39. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Julai, 2022 hadi Machi, 2023 Mahakama ya Ardhi imepokea jumla ya mashauri mapya **165** ambayo yamefunguliwa katika Mahakama za Unguja na Pemba. Aidha, Mahakama imeendelea kusikiliza mashauri hayo pamoja na ya awali ambapo jumla ya mashauri **160** yametolewa uamuzi, sawa na wastani wa **asilimia 73** ya lengo la kuamua mashauri **220** kwa kipindi cha miezi tisa (9). Kwa ufafanuzi zaidi angalia **Kiambatinisho F2.**

ii. Kutoa Elimu kwa jamii

40. Mheshimiwa Spika, Mahakama ya Ardhi imeendelea kutoa elimu kwa jamii juu ya umuhimu wa matumizi bora ya ardhi pamoja na kufuata Sheria mbalimbali za ardhi ili kuepuka migogoro nchini. Elimu hiyo ilitolewa kupitia vipindi maalumu vya "Televisheni" vilivyorushwa moja kwa moja (live) na ZBC pamoja na kushiriki katika programu ya kuwafikia wananchi (Outreach Program) iliyofanyika katika Vijiji vya Nungwi na Tumbatu kwa Mkoa wa Kaskazini Unguja na Paje kwa Mkoa wa Kusini Unguja.

41. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2022//2023 Mahakama ya Ardhi ilikadiriwa kukusanya jumla ya **TZS Milioni 10.00** ambapo hadi kufikia Machi 2022 ilifanikiwa kukusanya jumla ya TZS Milioni 9.032 sawa na **asilimia 90** ya makadirio.

Kwa upande wa Matumizi Mahakama ya Ardhi ilipangiwa kutumia jumla ya **TZS Millioni 584.000** kwa ajili ya utekelezaji wa kazi za Mahakama ya Ardhi. Hadi kufikia Machi, 2023 fedha zilizopatikana ni **TZS Milioni 297.582** ambapo **TZS Milioni 241.492** kwa ajili ya mishahara sawa na **asilimia 94** na **TZS Milioni 56.089** kwa ajili ya matumizi ya kawaida sawa na **asilimia 17** ya makadirio ya fedha zilizopangwa.

OFISI YA MTHAMINI MKUU WA SERIKALI

42. Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Mthamini Mkuu wa Serikali imeanzishwa kwa Sheria namba 5 ya mwaka 2015 kwa madhumuni ya kuhakikisha usimamizi mzuri wa uthaminishaji mali kwa malengo mbalimbali ya Sekta

ya umma, biashara na wananchi kwa ujumla. Kazi kuu ya Mthamini Mkuu ni kuthibitisha kazi za uthamini zinazofanywa nchini na Wathamini wa Taasisi za Serikali na Taasisi binafsi.

43. Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha 2022/2023 Ofisi ya Mthamini Mkuu wa Serikali imetekeleza kazi zifuatazo: -

i. Kuthibitisha ripoti za uthamini wa rasilimali kwa madhumuni mbalimbali; ambapo jumla ya ripoti 431 zimethibitishwa ambapo kati ya hizo 64 ni ripoti za uthamini mali kwa ajili ya mikopo (Morgage purpose), 103 ripoti za uthamini mali kwa ajili ya thamani (Market Value Determination), 211 ripoti za uthamini mali kwa ajili ya mirathi (Inheritance purpose) na 53 ripoti za uthamini mali kwa ajili ya fidia (Compensation purpose). Utekelezaji wa Shughuli hii hutegemea maombi yanayowasilishwa.

ii. Kutoa elimu ya Uthamini kwa wadau mbalimbali wa uthamini kupitia mikutano mbalimbali na vyombo vya habari kwa ajili ya kukuza ufahamu na umuhimu wa uthaminishaji wa mali kwa malengo tofauti, mfano uthamini kwa ajili ya fidia, uthamini kwa mikopo Benki, uthamini kwa ajili ya mirathi, uthamini kwa ajili ya uhaulishaji ardhi, uthamini kwa ajili ya bima, n.k.

iii. Kuendelea kusajili Wathamini na kuwapatia leseni; ambapo hadi kufikia Machi 2023 Ofisi ya Mthamini Mkuu wa Serikali imepokea maombi ya wathamini 11

na Kampuni 4 za uthamini ili kuwatambua wathamini na Kampuni za uthamini zinazofanya kazi Zanzibar na kuwapatia leseni.

44. Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Mthamini Mkuu wa Serikali ilikadiriwa kukusanya jumla ya **TZS Milioni 250.** Hadi kufikia Machi, 2023 ilifanikiwa kukusanya jumla ya **TZS Milioni 219.06** sawa na **asilimia 87.06** ya makadirio.

Kwa Upande wa Matumizi Ofisi ilipangiwa kutumia jumla ya **TZS Milioni 162.4.** Hadi kufikia Machi, 2023 fedha zilizopatikana ni **TZS Milioni 42.8** sawa na **asilimia 26** ya makadirio ya zilizopangwa.

FUNGU N04: KAMISHENI YA ARDHI

45. Mheshimiwa Spika, Kamisheni ya Ardhi imeanzishwa kwa Sheria Namba 6 ya Mwaka 2015. Lengo la kuanzishwa ni kuleta ufanisi zaidi katika kusimamia Sheria za Sekta ya Ardhi pamoja na kuziunganisha Idara zote zinazosimamia matumizi na maendeleo ya ardhi.

46. Mheshimiwa Spika, kwa Mwaka wa Fedha 2022/23 Kamisheni ya Ardhi imetekeleza kazi zifuatazo:-

i. Utawala na Uendeshaji

a. Jumla ya wafanyakazi 16 wamepatiwa mafunzo ya ndani yanayohusu mambo mbali ya utendaji wa majukumu yao na wafanyakazi 7 wamepatiwa fursa ya kujiunga na mafunzo ya muda mrefu.

b. Kusimamia maslahi ya Wafanyakazi ambapo stahiki zimetolewa kwa wafanyakazi 32 ikiwemo likizo na malipo baada ya saa za kazi.

ii. Ugawaji na Usimamizi wa Ardhi

a. Kamisheni imetayarisha Hati 442 (hati 344 kwa Unguja na 98 kwa Pemba), Aidha mikataba ya Ukodishaji Ardhi 166 imetayarishwa (mikataba 159 kwa Unguja na 7 kwa Pemba).

b. Kufanya ukaguzi wa maeneo 83 (Unguja 60 na Pemba 23) ya Ardhi za ukodishwaji.

c. Jumla ya maeneo 174 ya ardhi ya eka tatu yalifanyiwa ukaguzi kwa upande wa Unguja.

d. Maeneo 165 ya uwekezaji yamekaguliwa (Unguja 102 na Pemba 63)

e. Kufanya kazi za uthamini, jumla ya kazi 916 za uthamini zimetekelezwa ambapo 575 ni kwa Unguja na 441 ni kwa Pemba.

f. Kuendelea na zoezi la Utambuzi wa maeneo (parcels) 1,819 (857 kwa Unguja na 962 kwa upande wa Pemba)

g. Jumla ya Hati 388 za utambuzi zimetayarishwa (Unguja 367 na 21 Pemba)

iii. Kuratibu na kusimamia Usajili wa Ardhi

a. Kufanya usajili wa maeneo (parcels) 398 (374 kwa Unguja na 24 kwa Pemba).

b. Idadi ya maeneo yaliyohakikiwa ni 439 (Unguja 414 na Pemba 25)

c. Idadi ya hati zilizolipiwa ada ya usajili wa ardhi 443 (Unguja 300 na 143 Pemba)

d. Idadi ya ripoti za mikutano za uhamasishaji wa usajili wa ardhi iliyotayarishwa 10 (Unguja 4 na Pemba 6).

e. Idadi ya kadi za usajili zilizotayarishwa ni 397 (unguja 284 na Pemba 113)

f. Idadi ya mifumo midogo (modules) ya usajili iliyotayarishwa ni 3

iv. Upimaji na Utoaji wa Ramani za Ardhi

a. Jumla ya viwanja 1,510 vimepimwa kwa ajili ya matumizi mbalimbali (1,049 kwa upande wa Unguja na 461 kwa upande wa Pemba).

b. Idadi ya maeneo 6 yaliyopimwa kwa ardhi ya akiba (Land Bank).

c. Jumla ya ramani 1,669 zimetolewa kwa matumizi mbali mbali. (435 kwa Unguja na 1234 kwa upande Pemba.)

d. Jumla ya Ripoti 9 za ukusanyaji wa taarifa za vipimo vya kupwa na kujaa maji ya Bahari zilizokwenda Hawaii nchini USA.

e. Idadi ya huduma za usafi (services) zilizofanywa katika kituo cha kupima kupwa na kujaa maji ya Bahari (Tide Gauge) ni 9.

v. Upangaji wa Miji na Matumizi ya Ardhi

a. Jumla ya miongozo (PGs) 637 ya ujenzi imetolewa na kupewa wananchi (475 Unguja na 162 Pemba).

b. Vibali vya ujenzi 276 vilitolewa (Unguja 239 na 37 Pemba).

c. Eneo la ukanda wa Paje – Jambiani limepangwa linasubiri kazi ya upimaji na kwa upande wa Pemba Eneo moja (1) la wazi limepangwa.

vi. Ukusanyaji na Uwekaji wa taarifa za Ardhi.

a. Jumla ya wataalamu 10 wamepatiwa mafunzo ya muda mfupi juu ya kazi za upimaji na ramani kwa upande wa Unguja.

b. Vikao vya wadau juu ya kutoa uelewa wa kazi za upimaji ardhi vimefanyika.

47. Mheshimiwa Spika, Kamisheni ya Ardhi Kamisheni ya Ardhi ilikadiriwa kukusanya jumla ya **TZS Bilioni 1.022** kutokana na vyanzo mbalimbali ambapo hadi kufikia Machi 2023 ilifanikiwa kukusanya jumla ya **TZS Bilioni 1.624** sawa na **asilimia 160** ya makadirio.

Kwa upande wa matumizi, Kamisheni ya Ardhi ilikadiriwa kutumia jumla ya **TZS Bilioni 4.216** kwa kazi za kawaida na mishahara (ambapo jumla ya **Bilioni 1.522** kazi za kawaida (OC) na **TZS Milioni 909.5** kwa ajili ya ruzuku ya Bodi ya Uhaulishaji wa Ardhi, na **TZS Bilioni 1.785** ya mishahara). Hadi kufukia Machi, 2023 fedha zilizopatikana ni **TZS Bilioni 2.631** ambapo **TZS Bilioni 2.116** kwa ajili

ya mishahara sawa na **asilimia 119** na **TZS Milioni 514.48** kwa ajili ya matumizi ya kawaida sawa na **asilimia 21** ya fedha zilizopangwa.

PROGRAMU KUU PN0203: MAENDELEO YA MAKAAZI

48. Mheshimiwa Spika, Programu hii ina jukumu la kuhakikisha upatikanaji wa makaazi salama na endelevu kwa wananchi na watumishi wa Serikali, pamoja na kuweka mazingira rafiki kwa wawekezaji wa sekta binafsi katika huduma ya makaazi. Programu hii inasimamiwa na Wakala wa Majengo, Shirika la Nyumba Zanzibar, Bodi ya Kondominio, Bodi ya Kudhibiti Kodi za Nyumba, Bodi ya Usajili Wasanifu, Wahandisi na Wakadiriaji Majengo na Bodi ya Usajili Wakandarasi.

PROGRAMU NDOGO YA MAENDELEO YA MAKAAZI

49. Mheshimiwa Spika, Programu ndogo hii ina lengo la kuwapatia watumishi wa umma na wananchi makaazi bora pamoja na kusimamia ujenzi unaozingatia viwango.

50. Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha 2022/2023, jumla ya **TZS Bilioni 17.821** ziliidhinishwa kutumika kwa utekelezaji wa Programu ya hii kwa kazi za kawaida na maendeleo. Hadi kufikia Machi, 2023 fedha zilizopatikana ni **TZS Milioni 663.972** kwa ajili ya matumizi ya kawaida sawa na **asilimia 36** ya makadirio na kwa upande kazi Maendeleo hakuna fedha iliyopatikana. Hivyo Programu hii kwa ujumla imepata **asilimia 4** ya utekelezaji wa fedha zote kwa kazi za kawaida na Maendeleo.

51. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2022/2023 Programu hii inatekelezwa na Taasisi zifuatazo: -

WAKALA WA MAJENGO

52. Mheshimiwa Spika, Wakala wa Majengo imeanzishwa kwa Tangazo la Kisheria (Legal Notice) Namba 50 ya Mwaka 2017. Jukumu la msingi la Wakala wa Majengo ni kusimamia na kuratibu miradi ya ujenzi na matengenezo ya Majengo ya Serikali ili kuhakikisha ubora wa majengo hayo, pia ina jukumu la kutoa huduma ya makaazi kwa Viongozi wa Serikali, Maafisa Wakuu Wandamizi wa Serikali na Watumishi wa Umma.

53. Mheshimiwa Spika, kwa mwaka wa fedha 2022/2023 Wakala wa Majengo imetekeleza kazi zifuatazo: -

a. Usimamizi wa Nyumba za Serikali zilizokabidhiwa kwa Wakala wa Majengo (Real Estate Management)

b. Huduma za Ushauri Elekezi (Construction Design and Supervision)

c. Huduma ya Karani wa Ujenzi (Clerk of Works)

d. Huduma za ujenzi (Construction)

e. Kufanya ukarabati wa Jengo la Afisi yake liliopo Amani Viwanda vidogo vidogo.

Kiambatanisho Nambari E1 kinaonyesha Miradi tofauti inayotekelezwa na Wakala wa Majengo na Kiambatanisho nambari E2 kinaonyesha utekelezaji wa miezi tisa wa usimamizi wa Nyumba.

54. Mheshimiwa Spika, kwa mwaka wa fedha 2022/2023 Wakala wa Majengo ilipangiwa kukusanya jumla ya **TZS Milioni 300.** Hadi kufikia Machi, 2023 jumla ya **TZS Milioni 103.098** zimekusanywa sawa na asilimia 34 ya makadirio.

Kwa upande wa matumizi Wakala wa Majengo ilipangiwa ruzuku ya **TZS Milioni 489.0** kwa kazi za kawaida ambapo hadi kufikia Machi, 2023 jumla ya **TZS Milioni 301.433** zimepatikana sawa **asilimia 62** ya fedha zilizopangwa.

BODI YA KONDOMINIO

55. Mheshimiwa Spika, Bodi hii imeanzishwa kwa Sheria ya Kondominio Namba 10 ya Mwaka 2010 ambayo imetokana na Sera ya Nyumba ya Mwaka 2008. Majukumu ya msingi ya Bodi ni kusajili, kuratibu na kusimamia matumizi ya pamoja kwa majengo yenye sehemu zinazomilikiwa na mtu zaidi ya mmoja.

56. Mheshimiwa Spika, kwa Mwaka wa Fedha 2022-2023 Bodi ya Kondominio imefanikiwa kutekeleza kazi zifuatazo:-

a. Kutoa huduma za uendeshaji wa Ofisi ambapo Bodi imenunua vifaa mbali mbali kwa ajili ya matumizi ya Ofisi. Huduma hizo ikiwemo kulipia umeme, mtandao na huduma ya ulinzi.

b. Bodi iliwapatia mafunzo Watendaji wawili wa sehemu ya Masjala kuhusiana na Utunzaji Siri na mtendaji mmoja wa kitengo cha Tehama alipata mafunzo kuhusiana na Ulinzi wa Mtandao

c. Kuendelea na hatua za usajili wa Kondominio kwa Unguja na Pemba. Ofisi imetoa jumla ya fomu mia mbili ishirini (220) za maombi mbali mbali ya usajili wa Kondominio.

d. Kufanya usajili wa Ramani nne (4) katika miradi ya Kondominio ambayo ni System Design Solutions Company LTD wa Mbweni, PGH Company LTD wa Jambiani, Zanzibar Villas LTD (Phase 2) wa Paje na Abdughafour Ismail Mohammed wa Mlandege.

e. Kufanya usajili wa Majengo/Mradi ya Kondominio (Condominium Registration) kwa Miradi mitatu (3) amabayo ni Zanzibar Villas LTD - Paje, PGH Company LTD wa Jambiani na Abdughafour Ismail Mohammed wa Mlandege.

f. Kufanya usajili wa Umiliki wa Sehemu/fleti (Unit Registration) mia mbili na kumi na sita (216) katika Nyumba za Maendeleo za Kilimani, Michenzani, Kikwajuni na Mombasa Kwa Mchina na Machomane.

g. Kufanya ukaguzi wa miradi mbali mbali ambapo jumla ya miradi kumi na mbili (12) ya Kondominio ilifanyiwa ukaguzi kwa ajili ya kuitambua.

h. Kutoa elimu kupitia vipindi mbali mbali vya redio pamoja na mikutano ya hadhara ya wakaazi wa wanaotumia majengo ya kondominio kuhusu ya Dhana ya Kondominio, Usajili na Usimamizi wa majengo ya Kondominio pamoja na kutoa matangazo ya usajili.

57. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2022/2023 Bodi ya Kondominio ilikadiria kukusanya jumla ya **TZS Milioni 325. 000** hadi kufikia Machi 2023 Bodi imeweza kukusanya jumla ya **TZS Milioni 288.00** sawa na **asilimia 89** ya makadirio.

Kwa upande wa matumizi Bodi ya Kondominio ilipangiwa ruzuku ya **TZS Milioni 240.00** kwa ajili ya utekelezaji wa kazi zake. Hadi kufikia Machi, 2023 fedha zilizoingizwa ni **TZS Milioni 173.860** ambazo ni sawa **asilimia 72** ya fedha zilizopangwa.

BODI YA KUDHIBITI KODI ZA NYUMBA

58. Mheshimiwa Spika, Bodi ya Kudhibiti Kodi za Nyumba imeanzishwa kwa Sheria ya Kudhibiti Kodi za Nyumba, Sura ya 98 ya Mwaka 1953 (Cap. 98 of 1953). Majukumu ya Msingi ya Bodi hii ni kusikiliza na kuyatolea uamuzi mashauri yanayotokana na migogoro ya upangishaji wa Nyumba za Serikali na Nyumba binafsi.

59. Mheshimiwa Spika, kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023 Bodi ya Kudhibiti Kodi za Nyumba imetekeleza kazi zifuatazo: -

i. Imepokea mashauri Ishirini na nne (24) kati ya hayo Unguja Ishrini na Mbili (22) na Pemba Mawili (02), hivyo kufanya Bodi hii kwa sasa kuwa na Mashauri 42.
ii. Imeweza kusikiliza mashauri Ishirini na Nane (28) kwa kipindi hicho.

iii. Imeweza kuyatolea maamuzi mashauri ya migogoro ya kodi za nyumba kwa Zanzibar Kumi na nne (14) kati ya hayo 12 Unguja na 2 Pemba.

iv. Bodi imeweza kutoa elimu kwa jamii kuhusu utendaji wa kazi za bodi kupitia vyombo vya habari na mikutano mbalimbali.

60. Mheshimiwa Spika, kwa mwaka wa fedha 2022/2023 Bodi ya Kudhibiti Kodi za Nyumba imepangiwa ruzuku ya **TZS Milioni 135.0** kwa ajili ya matumizi ya kazi za kawaida. Hadi kufikia Machi, 2023 fedha zilizopatikana ni **TZS Milioni 36.600** ambazo sawa na **asilimia 27** ya fedha zilizopangwa.

BODI YA USAJILI WASANIFU WAHANDISI NA WAKADIRIAJI MAJENGO

61. Mheshimiwa Spika, Bodi hii imeanzishwa kwa Sheria ya Usajili wa Wasanifu, Wahandisi na Wakadiriaji Majengo namba 5 ya Mwaka 2008. Majukumu ya msingi ya Bodi hii ni kusimamia, kudhibiti na kuwaendeleza Wataalamu wa ujenzi ili waweze kufanya kazi zao kwa utaalamu na viwango vinavyotakiwa.

62. Mheshimiwa Spika, kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023 Bodi ya Usajili Wasanifu, Wahandisi na Wakadiriaji Majengo imetekeleza kazi zifuatazo: -

i. Kusajili Miradi 192 katika maeneo mbali mbali ya Ujenzi kwa Unguja na Pemba, miradi hiyo inajumuisha Miradi ya Majengo ya Biashara, Nyumba za Makaazi, Hoteli, Skuli, Nyumba za Ibada na mengineyo.

ii. Kukagua Miradi ya ujenzi kwa maeneo 20 ya miradi ya ujenzi Unguja na Pemba.

63. Mheshimiwa Spika, kwa mwaka wa fedha 2022/2023 Bodi ya Usajili Wasanifu, Wahandisi na Wakadiriaji Majengo ilipangiwa kukusanya jumla ya **TZS Milioni 662.069.** Hadi kufikia Machi, 2023 jumla ya **TZS Milioni 246.103** zimekusanywa ambazo sawa na **asilimia ya 37** ya makadirio.

Kwa upande wa Matumizi Bodi ya Usajili Wasanifu, Wahandisi na Wakadiriaji Majengo imepangiwa ruzuku ya **TZS Milioni 676.000** kwa ajili ya matumizi ya kazi za kawaida. Hadi kufikia Machi, 2023 fedha zilizopatikana ni **TZS Milioni 81.025** ambazo sawa na **asilimia 12** ya fedha zilizopangwa.

BODI YA USAJILI WA WAKANDARASI

64. Mheshimiwa Spika, Bodi ya Usajili wa Wakandarasi imeanzishwa kwa Sheria ya Usajili wa Wakandarasi Namba 6 ya Mwaka 2008. Majukumu ya msingi ya Bodi hii ni kusimamia Kampuni za ujenzi na miradi ya ujenzi inayotekelezwa nchini ili kuzingatia viwango na usalama.

65. Mheshimiwa Spika, kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023 Bodi ya Usajili wa Wakandarasi imetekeleza kazi zifuatazo:-

i) Kusajili miradi inayotekelezwa na Wakandarasi waliosajiliwa ipatayo Mia Moja Thalathini na Nane (138).

ii) Kukagua Kampuni 21, ambapo kampuni 15 zimekamilisha masharti ya kusajiliwa na Kampuni 6 ambazo zinaomba kupandishwa madaraja

iii) Kuwahamasisha Wakandarasi juu ya kuisajili miradi yao katika Bodi pamoja na kufuata Sheria na Kanuni za Bodi.

66. Mheshimiwa Spika, kwa mwaka wa fedha 2022/2023 Bodi ya Wakandarasi ilipangiwa kukusanya jumla ya **TZS Bilioni 1.445** Hadi kufikia Machi, 2023 jumla ya **TZS Milioni 307. 832** zimekusanywa ambazo sawa na **asilimia 21** ya makadirio.

Kwa Upande wa Matumizi Bodi ya Wakandarasi imepangiwa ruzuku ya **TZS Milioni 281.600** kwa ajili ya matumizi ya kazi za kawaida. Hadi kufikia Machi, 2023 fedha zilizopatikana ni **TZS Milioni 71.053** ambazo sawa na **asilimia 25** ya makadirio ya fedha zilizopangwa.

67. Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha 2022/2023, jumla ya **TZS Bilioni 17.821** ziliidhinishwa kutumika kwa utekelezaji wa Programu ya Maendeleo ya Makaazi kwa kazi za kawaida na maendeleo. Hadi kufikia Machi, 2023 fedha zilizopatikana ni **TZS Milioni 639.704** sawa na **asilimia 4** ya makadirio kwa mwaka na **asilimia 4** kwa ulinganisho wa fedha zilizopangwa miezi tisa (9).

TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA SHIRIKA LA NYUMBA ZANZIBAR

68. Mheshimiwa Spika, Shirika la Nyumba Zanzibar ni taasisi inayojitegemea iliyoanzishwa kwa Sheria Namba 6 ya Mwaka 2014. Taasisi hii imepewa Mamlaka ya kusimamia na kuendeleza sekta ya nyumba Zanzibar kwa

kuchangia katika ukuaji wa uchumi na Maendeleo ya makaazi kwa wananchi wa Zanzibar ili kwenda sambamba na mahitaji ya nyumba kutokana na ongezeko la watu na mahitaji, pamoja na utoaji wa huduma za ujenzi, ushauri na uwekezaji.

69. Mheshimiwa Spika, kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023 Shirika la Nyumba katika Programu hii ndogo imetekeleza kazi zifuatazo:-

i. Kukamilisha kwa matengenezo ya awamu ya tatu (Phase III) ya nyumba za maendeleo 24 za Bloki No.1 ngazi namba 3. Aidha hadi kufikia Machi 30 2023 kazi hiyo imefikia asilimia 80%.

ii. Kuendelea na Matengenezo madogo madogo ya nyumba namba 334 Shangani, nyumba namba 1891 Mkunazini na nyumba namba 1508 Kiponda

iii. Matengenezo makubwa ya awamu ya pili (phase II) ya nyumba namba 1699/1705 Mkunazini (Mnadani) yamefikia katika hatua ya ununuzi wa vifaa kwa ajili ya kuanza kazi.

iv. Ujenzi wa jengo la makaazi na biashara Mombasa (Kwa Mchina) ambapo Shirika linaendelea na hatua ya ujenzi wa nyumba 72.

v. Ujenzi wa Nyumba ya makaazi na biashara Mkungu Malofa (Mabatini) umeshaanza na uko hatua ya kumwaga zenge ya juu ya msingi.

vi. Shirika limefanya uthamini wa nyumba zake zilizopo Mombasa kwa Mchina.

vii. Kazi ya kukagua nyumba za Shirika imefanyika na kuwapatia mikataba mipya wapangaji wa maduka ya Mnadani awamu ya kwanza.

viii. Wafanyakazi kumi (10) wa fani tofauti wamepatiwa mafunzo ya muda mfupi ndani ya nchi.

ix. Kufanya ukaguzi wa kawaida wa nyumba za Shirika ili kuwatambua wapangaji halisi, kufuatilia madeni, mikataba ya upangishwaji na kujua changamoto zilizopo.

x. Mikataba 197 mipya ya ukodishaji kwa wapangaji wa nyumba za Shirika Unguja na Pemba imeingiwa.

xi. Kuratibu mikutano mitatu ya kuhamasisha wapangaji kulipa kodi na matumizi sahihi ya nyumba za Shirika kwa wapangaji wa nyumba za Maendeleo Madungu (Pemba), Mpapa na Makunduchi

70. Mheshimiwa Spika, kwa Mwaka wa Fedha 2022/23 Shirika la Nyumba Zanzibar lilikadiria kukusanya Jumla ya **TZS Bilioni 9.902** kutoka vyanzo vyake mbalimbali vya mapato. Hadi kufikia Machi, 2023 fedha zilizokusanywa ni **TZS Bilioni 2,026** ambazo zinazotokana na vyanzo vyake vya ndani ikiwemo kodi, mikataba, dhamana na tozo nyenginezo sawa **asilimia 20.46%** ya makadirio ya makusanyo ya mwaka.

Aidha, Shirika halikufanikiwa kukusanya **TZS Bilioni 3.00** zilipangwa kukusanywa kutokana na mkopo kutoka taasisi za kifedha kwa sababu ya kutokamilika kwa taratibu za Benki, **TZS Bilioni 3.00** zilipangwa kukusanywa kutokana na mauzo ya nyumba hii imetokana

na kuchelewa kwa Mradi wa nyumba za bei nafuu Kwa Mchina na **TZS Milioni 150.00** zilipangwa kukusanywa kutokana na kazi za ujenzi na ushauri elekezi, hadi kufikia Machi 2023 Shirika halikufanikiwa kupata kazi za zinazotokana na ujenzi na ushauri elekezi.

Kwa upande wa matumizi, katika mwaka wa fedha 2022-2023 Shirika lilikadiria kutumia jumla ya **TZS Bilioni 8.898** kwa kazi za kawaida, ujenzi na matengenezo, ambapo hadi kufikia Machi 2023 jumla ya **TZS Bilioni 2.004** zimetumika sawa na **asilimia 23%** ya makadirio. Hata hivyo matumizi hayo yanaonekana kuwa madogo ukilinganisha na matarajio ya kazi zilizopangwa, hii imetokana na kuchelewa kuanza kwa miradi ya ujenzi na baadhi ya matengenezo ya nyumba ikiwemo mradi wa ujenzi wa nyumba za makaazi na biashara Mombasa (Kwa Mchina) na matengenezo ya nyumba nam.1699/1705 Mkunazini (Mnadani).

CHANGAMOTO NA HATUA ZA UTATUZI WAKE

71. Mheshimiwa Spika, licha ya kuwa Wizara imefanikiwa kutekeleza majukumu yake mbalimbali kwa kiasi kikubwa kwa mwaka wa fedha 2022-23. vilevile Wizara imekabiliwa na changamoto mbalimbali kama ifuatavyo: -

i. Kuwepo kwa ongezeko la uvamizi na ujenzi holela katika maeneo mbalimbali ya Zanzibar ambapo Wizara imefanya vikao mbali mbali na Wadau wote wanaoshirikiana katika utoaji wa vibali vya ujenzi kwa lengo la kuhakikisha kuwa vibali vya ujenzi vinatolewa na Kamati ya kusimamia na kudhibiti Ujenzi (DCU).

ii. Kuwepo kwa Migogoro ya Ardhi ya muda mrefu ambayo Wizara inaendelea kuchukua hatua za kuitafutia ufumbuzi kupitia kamati ya ufuatiliaji wa migogoro ya Wizara pamoja na kutoa elimu kwa jamii juu ya umuhimu wa matumizi na utawala bora wa ardhi ili kuweza kutatua changamoto za migogoro hiyo na kupunguza ujenzi holela

iii. Kuwepo kwa uelewa mdogo wa utaratibu wa uwasilishwaji wa migogoro ya kodi za nyumba kwa wananchi ambapo Wizara kupitia Bodi ya Kudhibiti kodi za nyumba inaendelea kutoa elimu kwa jamii kupitia vyombo mbalimbali vya habari.

iv. Kuwepo kwa kiwango kikubwa cha ardhi ambayo haijafanyiwa utambuzi na kusajiliwa kulingana na malengo ya usajili. Wizara inaendelea na zoezi la utambuzi wa ardhi katika maeneo mbalimbali ya Zanzibar.

v. Kuwepo kwa upungufu wa wataalamu katika fani zinazohusiana na ardhi pamoja na Nyumba. Katika kutatua changamoto hiyo Wizara inaendelea kuwajengea uwezo wafanyakazi wake kwa kuwapatia ujuzi stahiki wa matumizi sahihi ya teknolojia na vifaa vinavyokwenda na wakati katika masuala ya ujenzi pamoja na kuratibu ajira mpya za wataalamu wa fani tofauti za ujenzi na usimamizi wa ardhi

vi. Uchakavu wa nyumba za Maendeleo na nyumba zinasimamiwa na Wakala wa Majengo Zanzibar. Wizara kupitia Bodi ya Kondominio inaendelea kushajihisha wananchi juu ya uundwaji wa jumuiya za Kondominio ambazo zitahusisha utunzaji wa nyumba zinazokaliwa

na watu wengi pamoja na kuendeleza ushirikiano na Wawekezaji na Taasisi mbalimbali ambao wamekuwa na dhamira ya dhati katika kuimarisha ushirikiano katika Sekta ya Ardhi, Nyumba na Makaazi.

MWELEKEO WA MAKADIRIO YA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2023/2024.

72. **Mheshimiwa Spika,** baada ya kutoa maelezo ya utekelezaji wa Bajeti ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023, sasa naomba kuwasilisha mwelekeo wa Bajeti yenye kuzingatia Programu ya Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024.

VIPAOMBELE VIKUU VYA WIZARA KWA MWAKA WA FEDHA 2023/2024.

73. **Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi kwa mwaka wa fedha 2023/2024 imejipangia kutekeleza bajeti yake kwa kuzingatia vipaombele vifuatavyo: -

i. Kujenga nyumba za bei nafuu katika maeneo mbalimbali ya Unguja na Pemba.

ii. Kuendelea na zoezi la kufanya utambuzi wa maeneo ya Unguja na Pemba ili kupunguza Migogoro ya ardhi na kudhibiti ujenzi holela nchini ikiwemo maeneo ya uwekezaji.

iii. Kuendelea na kuandaa Mipango ya matumizi ya ardhi ya Miji mbalimbali (Local Area Development Plans) kwa Unguja na Pemba

74. **Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi imepangiwa kutumia jumla ya **TZS Bilioni 17.01** kati ya hizo **TZS Bilioni 7.023** ni kwa ajili ya utekelezaji wa kazi za kawaida kwa fungu la Wizara, ambapo kati ya fedha hizo jumla ya **TZS Bilioni 4.079** zimetengwa kwa ajili ya mishahara kwa Idara zilizo chini ya Wizara, **TZS Bilioni 1.456** kwa ajili ya matumizi ya kawaida ya uendeshaji wa ofisi kwa Idara zilizo chini ya Wizara na **TZS Bilioni 1.489** ni ruzuku ya matumizi mengineyo kwa ajili ya Taasisi za Wizara.

Vilevile kwa upande wa fungu la Kamisheni ya Ardhi imepangiwa kutumia jumla ya **TZS Bilioni 9.98** kwa ajili ya kazi za kawaida, ruzuku ya matumizi mengineyo, mishahara na kazi za maendeleo ambapo kati ya hizo **TZS Bilioni 4.662** kwa ajili ya kazi za kawaida, **TZS Bilioni 4.55** kwa ajili ya kazi za Maendeleo na **TZS Milioni.773.07** kwa ajili ya ruzuku ya uhaulishaji wa ardhi.

75. **Mheshimiwa Spika,** aidha, kwa mwaka wa Fedha 2023/2024 Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi imepangiwa kukusanya mapato ya jumla ya **TZS Bilioni 7.505** zinazoingia katika mfuko Mkuu wa Serikali, kati ya hizo Jumla ya **TZS Bilioni 4.754** kwa ajili ya makusanyo yanayotokana na vyanzo vya fungu la Wizara na jumla ya **TZS Bilioni 2.750** kwa ajili ya makusanyo yanayotokana na vyanzo vya Fungu la Kamisheni ya Ardhi. Kwa ufafanuzi zaidi angalia viambatisho vya D1 – D4

76. Mheshimiwa Spika, Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi itatekeleza kazi zake kupitia vipaombele ambavyo vilivyotajwa hapo juu kupitia Programu Kuu tatu kama ifuatavyo: -

a. Programu PN0201: Uendeshaji na Uratibu wa Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi

b. Programu PN0202: Usimamizi wa Ardhi

c. Programu PN0203: Maendeleo ya Makaazi

77. Mheshimiwa Spika, naomba sasa uniruhusu kutoa maelezo kuhusu Programu Kuu na Programu ndogo za Wizara kama ifuatavyo:-

PROGRAMU KUU PN0201: UENDESHAJI NA URATIBU WA WIZARA YA ARDHI NA MAENDELEO YA MAKAAZI

78. Mheshimiwa Spika, Programu hii inajukumu la kusimamia na kuratibu utekelezaji wa Kazi za Wizara ambapo matokeo ya muda mrefu yanayotarajiwa ni kukuza ufanisi katika utawala wa rasilimali Ardhi na huduma za Makaazi kwa jamii. Programu hii itasimamiwa na Idara ya Mipango, Sera na Utafiti, Idara ya Uendeshaji na Utumishi, na Afisi Kuu Pemba ambapo jumla ya TZS Bilioni 4.947 zinatarajiwa kutumika katika utekelezaji wake. Programu hii imegawanyika katika Programu ndogo kama ifuatavyo:-

a. **Programu ndogo SN020101:** Uratibu wa Mipango, Sera na Utafiti
b. **Programu ndogo SN020102:** Utawala na Uendeshaji
c. **Programu ndogo SN020103:** Uratibu wa Shughuli za Wizara Pemba

PROGRAMU NDOGO YA URATIBU WA MIPANGO, SERA NA UTAFITI

79. **Mheshimiwa Spika,** madhumuni ya Programu ndogo hii ni uratibu wa shughuli za kazi za Wizara kwa Ufanisi. Kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 Programu hii imepanga kutekeleza kazi zifuatzo:-

i. Kuratibu uandaji wa Sera ya Makaazi na kuendelea kukamilisha Sera ya Mipango Miji na vijiji.

ii. Kuratibu uandaaji wa Mipango ya Wizara na Taasisi zake,

iii. Kuratibu mapitio ya Sheria nne (04) zilizo chini ya Taasisi za Wizara,

iv. Kufuatilia na kutathmini utekelezaji wa kazi na Miradi mbalimbali ya Wizara,

v. Kuratibu utekelezaji wa kazi zinazofanywa na Kamati ya kudhibiti ujenzi (DCU),

vi. Kuratibu uandaaji wa ramani za kidigitali za Anuani ya Makaazi pamoja na kuendeleza taarifa za Sensa ya Majengo,

vii. Kufanya Tafiti kwa ajili ya kuwezesha utoaji wa huduma bora katika Sekta za Wizara na

viii. Kuratibu Vikao vya ushirikiano baina ya Taasisi za SMZ na SMT.

80. Mheshimiwa Spika, vilevile, kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 Wizara Kupitia Proramu hii imepanga kuratibu utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo katika Sekta ya Ardhi na Makaazi inayohusisha Mradi wa Utayarishaji wa Mpango wa Matumizi ya Ardhi na Miradi wa ujenzi wa nyumba za bei nafuu.

81. Mheshimiwa Spika, kwa mwaka wa fedha 2023/2024 Programu hii imepangiwa kukusanya jumla ya **TZS Bilioni 1.476** kutokana na mapato yatokayo na utoaji wa Vibali vya ujenzi kupitia Kamati ya Usimamizi na Udhibiti Ujenzi (DCU).

82. Mheshimiwa Spika, ili kuiwezesha Programu hii kutekeleza majukumu yake kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024, naliomba Baraza lako kuidhinisha jumla ya **TZS Milioni 744.430** kwa ajili ya kazi za kawaida na mishahara, ambapo **TZS Milioni 557.018** kwa ajili ya matumizi ya kawaida na **TZS Milioni 187.412** kwa ajili ya mishahara.

PROGRAMU NDOGO YA UTAWALA NA UENDESHAJI

83. Mheshimiwa Spika, kwa mwaka wa fedha 2023/2024 programu hii imepanga kuendeleza kazi zifuatazo:-

i. Kuratibu shughuli za uendeshaji na usimamizi wa rasilimali za Wizara

ii. Kuwajengea uwezo wafanyakazi na kuwapatia stahiki zao kwa mujibu wa taratibu za Utumishi,

iii. Kuhakikisha kuwepo kwa watendaji wa kutosha na wenye sifa,

iv. Kufanya mapitio ya mkataba wa huduma kwa wateja,

v. Kuratibu mapitio ya miundo na majukumu ya Taasisi zilizo chini ya Wizara ili kuleta ufanisi zaidi katika utekelezaji wa kazi na kuimarisha ushirikiano baina ya Wizara.

84. Mheshimiwa Spika, ili kuiwezesha Programu hii kutekeleza majukumu yake kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024, naliomba Baraza lako kuidhinisha jumla ya **TZS Bilioni 3,149** kwa ajili ya kazi za kawaida na mishahara, ambapo **TZS Milioni 405.001** kwa ajili ya kazi za kawaida na **TZS Bilioni 2.744** kwa ajili ya Mishahara.

PROGRAMU NDOGO YA URATIBU WA SHUGHULI ZA WIZARA PEMBA

85. Mheshimiwa Spika, madhumuni ya Programu hii ni Uratibu na Utekelezaji wa shughuli za Wizara Pemba, ambapo kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 Programu hii imepanga kutekeleza kazi zifuatazo:-

i. Kuratibu shughuli za Wizara kwa upande wa Pemba

ii. Kuimarisha kazi na usimamizi wa mipango, bajeti na ufuatiliaji wa Programu na miradi ya Maendeleo ya Wizara Pemba.

iii. Kuimarisha mazingira bora ya kufanyia kazi kwa wafanyakazi.

86. Mheshimiwa Spika, kwa mwaka wa fedha 2023/2024 Programu hii imepangiwa kukusanya jumla ya **TZS Milioni 98.00** kutokana na vyanzo vyake mbalimbali vya mapato.

87. Mheshimiwa Spika, ili kuiwezesha Programu hii kutekeleza majukumu yake kwa mwaka wa fedha 2023/2024, naliomba Baraza lako kuidhinisha jumla ya **TZS Bilioni 1.054** kwa ajili ya kazi za kawaida na mishahara, ambapo **TZS Milioni 248.581** kwa ajili ya kazi za kawaida na **TZS Milioni 805.423** kwa ajili ya mishahara.

PROGRAMU KUU PN0202: USIMAMIZI WA ARDHI

88. Mheshimiwa Spika, Programu hii ina jukumu la kuhakikisha usalama wa matumizi na umiliki wa ardhi (Security of Land Tenure). Matokeo ya muda mrefu yanayotarajiwa ni kuwa na matumizi ya ardhi yaliyo bora Kiuchumi na Kijamii. Programu hii inasimamiwa na Kamisheni ya Ardhi, Afisi ya Mthamini Mkuu wa Serikali pamoja na Mahakama ya Ardhi.

89. Mheshimiwa Spika, kwa mwaka wa fedha 2023/2024 Programu hii imepangiwa kukusanya jumla ya **TZS Milioni 280** kutokana na vyanzo vyake mbalimbali vya mapato.

90. Mheshimiwa Spika, ili kuiwezesha Programu ya Usimamizi wa Ardhi kutekeleza majukumu yake kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024, naliomba Baraza lako kuidhinisha jumla ya **TZS Milioni 801.283** kwa ajili ya utekelezaji wa kazi za kawaida mishahara na ruzuku ya matumizi mengineyo kwa Ofisi ya Mthamini Mkuu wa Serikali, ambapo **TZS Milioni 245.00** kwa ajili ya kazi za kawaida, **TZS Milioni 342.604** kwa ajili ya mshahara wa Mahakama ya Ardhi na **TZS Milioni 213.680** kwa ajili ya ruzuku ya matumizi mengineyo.

91. Mheshimiwa Spika, Programu hii ina Programu ndogo ifuatayo:-

PROGRAMU NDOGO YA USIMAMIZI WA ARDHI

92. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2023/2024 Programu hii imelenga kutekeleza shughuli zote zinazohusiana na masuala ya Ardhi na inatekelezwa na Taasisi zifuatazo: -

MAHAKAMA YA ARDHI

93. Mheshimiwa Spika, kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 Mahakama ya Ardhi kupitia programu hii ndogo imepanga kutekeleza kazi zifuatazo:-

i. Kuendelea kupokea, kusikiliza na kutoa maamuzi ya mashauri yanayohusiana na migogoro ya ardhi iliyowasilishwa Mahakamani, kwa mwaka wa fedha 2023/ 2024 Mahakama imepanga kuyatolea uamuzi mashauri 290 kwa mwaka ambapo Unguja mashauri 195 na Pemba mashauri 95.

ii. Kuendelea kutoa elimu kwa jamii kuepuka kujiingiza kwenye migogoro ya ardhi kwa kufuata Sheria za ardhi.

iii. Kujenga mazingira bora ya kufanyia kazi kwa kufanya ukarabati wa Mahakama ya Ardhi ya Mwanakwerekwe

94. Mheshimiwa Spika, kwa mwaka wa fedha 2023/2024 Mahakama ya Ardhi imepangiwa kukusanya jumla ya **TZS Milioni 10.00** kutokana na vyanzo vyake mbalimbali vya mapato. Aidha ili kuiwezesha Mahakama ya Ardhi kutekeleza majukumu yake kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024, naliomba Baraza lako kuidhinisha **TZS Milioni 587.604** kwa ajili ya utekelezaji wa kazi zake za kawaida na Mishahara.

OFISI YA MTHAMINI MKUU WA SERIKALI

95. Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Mthamini Mkuu wa Serikali ina jukumu la kuhakikisha usimamizi mzuri wa kazi za uthamini kwa Serikali, Sekta binafsi na Wananchi kwa ujumla kwa kuhakiki na kuidhinisha kazi zote za uthamini nchini. Kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 Ofisi ya Mthamini Mkuu wa Serikali imepanga kutekeleza kazi zifuatazo: -

i. Kuhakiki na kuidhinisha ripoti 520 za uthamini wa rasilimali kwa madhumuni mbalimbali.

ii. Kuendelea kusajili na kuwapatia leseni Wathamini.

iii. Kuandaa miongozo mbali mbali ya uthamini ikiwemo muongozo wa uthamini wa fidia Zanzibar, Muongozo wa masafa ya mazao na miti, Muongozo wa thamani za

Ardhi na Majengo, pamoja na Muongozo wa viwango vya thamani ya haki ya Ardhi. Kutayarisha kanuni ya viwango vya thamani ya Ujenzi na Ardhi.

iv. Kutoa elimu ya uthamini kwa wadau mbalimbali kwa vyombo vya habari (kupitia vipindi vya Televisheni, Redio) pamoja na Mikutano kwa Taasisi za Serikali na Sekta Binafsi.

96. Mheshimiwa Spika, kwa mwaka wa fedha 2023/2024 Ofisi ya Mthamini Mkuu wa Serikali imepangiwa kukusanya jumla ya **TZS Milioni 270.00** kutokana na vyanzo vyake mbalimbali vya mapato. Aidha ili kuiwezesha Ofisi ya Mthamini Mkuu wa Serikali kutekeleza majukumu yake kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024, naliomba Baraza lako kuidhinisha **TZS Milioni 213. 680** kwa ajili ya utekelezaji wa kazi zake za kawaida.

KAMISHENI YA ARDHI

97. Mheshimiwa Spika, kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi kupitia Kamisheni ya Ardhi, imepanga kutekeleza kazi zifuatazo:-

i. Kuendelea na usimamizi wa dhana nzima ya utawala wa ardhi kwa kufanya yafutayo; -

- Kutayarisha hati za haki za matumizi ya ardhi, vitambulisho vya eka tatu na mikataba ya ukodishwaji wa ardhi.

- Kufanya ukaguzi, ufuatiliaji na usimamizi wa maeneo ya eka tatu (3) ili kuzuia uvamizi kwa lengo la kuyadhibiti maeneo hayo.

- Kufanya uhakiki wa hati za matumizi ya ardhi ili kutambua uhalali wa matumzi ya hati hizo kwa kufuata masharti yaliyowekwa.

- Kufanya ukaguzi na ufuatiliaji wa maeneo yote ya uwekezaji sambamba na kuhakiki mikataba ya ukodishaji wa ardhi (lease agreements) ili kutambua usahihi wa malipo ya kodi ya ardhi kwa wawekezaji wote.

- Kuratibu na kusimamia zoezi la uhaulishaji wa ardhi

ii. Kuimarisha zoezi la utambuzi na usajili wa ardhi.

iii. Kuandaa mipango ya matumizi ya ardhi (Local Area Development Plans). ya miji midogo minne (4) ya Nungwi, Kitogani, Mahonda na Konde.

iv. Kuandaa miongozo ya ujenzi (Planning Policy Guidelines – PPG) pamoja na kufuatilia utekelezaji wake.

v. Kuendelea na upimaji wa maeneo ya viwanda na akiba (Land Banks).

vi. Kutayarisha ramani za ardhi na kuimarisha mfumo wa uhifadhi wa ramani hizo (digitalization).

vii. Upimaji wa juu ya bahari (Hydrographical Survey), usimamizi wa vipimo vya miinuko wa Ardhi unayotokana kupwa na kujaa maji ya bahari na kumbukumbu za upimaji na ramani.

viii. Kuimarisha alama za vianzio vya upimaji (Control Survey)

ix. Kuimarisha kituo cha Ramani (Workstation)

98. Mheshimiwa Spika, kwa mwaka wa fedha 2023/2024 Kamisheni ya Ardhi (COLA) imepangiwa kukusanya jumla ya **TZS Bilioni 2.750** kutokana na vyanzo vyake mbalimbali vya mapato. Aidha, ili kuiwezesha Kamisheni ya Ardhi kutekeleza majukumu yake kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024, naliomba Baraza lako kuidhinisha **TZS Bilioni 9.985** kwa ajili ya utekelezaji wa kazi za kawaida, ruzuku ya matumizi mengineyo, mishahara pamoja na kazi za Maendeleo.

PROGRAMU KUU PN0203: MAENDELEO YA MAKAAZI

99. Mheshimiwa Spika, Programu hii ina jukumu la kuimarisha Makaazi bora na salama kwa kuanzisha na kuendeleza miji ya kisasa pamoja na usimamizi wa shughuli za ujenzi Nchini. Matokeo ya muda mrefu yanayotarajiwa ni kuwepo kwa makaazi bora na kuimarika kwa miji yetu. Programu hii inasimamiwa na Wakala wa Majengo, Shirika la Nyumba, Bodi ya Kondominio, Bodi ya Kudhibiti Kodi za Nyumba, Bodi ya Usajili Wasanifu, Wahandisi na Wakadiriaji Majengo na Bodi ya Usajili Wakandarasi.

PROGRAMU NDOGO YA MAENDELEO YA MAKAAZI

100. Mheshimiwa Spika, Programu hii ina jukumu la kuhakikisha upatikanaji wa makaazi salama na endelevu kwa wananchi na watumishi wa ngazi zote wa Serikali, pamoja na kuweka mazingira rafiki kwa wawekezaji wa sekta binafsi katika huduma ya makaazi.

WAKALA WA MAJENGO

101. Mheshimiwa Spika, kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 Wakala wa Majengo imepanga kutekeleza kazi zifuatazo:-

i. Kutoa huduma za ushauri elekezi, usimamizi wa majengo na udhibiti wa viwango na ubora katika miradi ya ujenzi wa majengo na miundombinu ya Serikali.

ii. Kujenga na kukarabati majengo na miundombinu inayohusiana na ujenzi wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

102. Mheshimiwa Spika, kwa mwaka wa fedha 2023/2024 Wakala wa Majengo imepangiwa kukusanya jumla ya **TZS Milioni 386.00** kutokana na vyanzo vyake mbalimbali vya mapato. Aidha, ili kuiwezesha Wakala wa Majengo kutekeleza majukumu yake kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024, naliomba Baraza lako kuidhinisha **TZS Milioni 473.200** kwa ajili ya utekelezaji wa kazi za kawaida.

BODI YA KONDOMINIO

103. Mheshimiwa Spika, kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 Bodi ya Kondominio imepanga kutekeleza kazi zifuatazo:-

i. Kuweka mazingira mazuri ya kazi kwa kuendelea na awamu ya tatu ya matengenezo ya Jengo la Ofisi, kutoa huduma za uendeshaji pamoja na kukuza uwezo wa kitaaluma kwa wafanyakazi wa Bodi.

ii. Kuendelea kufanya usajili wa miradi mipya ya Kondominio Ramani, Majengo, Sehemu/fleti na Jumuiya za Kondominio Unguja na Pemba.

iii. Kufanya ukaguzi na uhakiki katika miradi ya Kondominio.

iv. Kusimamia uanzishaji na uendeshaji wa Jumuiya za Kondominio katika uendeshaji na usimamizi wa maeneo ya pamoja kwa nyumba ambazo zimeshasajili.

v. Kuendelea kutoa elimu kwa Wadau pamoja na Wananchi kuhusu dhana nzima ya kondominio pamoja na usimamizi na uendeshaji wa Jumuiya zake.

104. Mheshimiwa Spika, kwa mwaka wa fedha 2023/2024 Bodi ya Kondominio imepangiwa kukusanya jumla ya **TZS Milioni 330.00** kutokana na vyanzo vyake mbalimbali vya mapato. Aidha, ili kuiwezesha Bodi ya Kondominio kutekeleza majukumu yake naliomba Baraza lako kuidhinisha jumla ya **TZS Milioni 168.00** kwa ajili ya utekelezaji wa kazi za kawaida.

BODI YA KUDHIBITI KODI ZA NYUMBA

105. Mheshimiwa Spika, kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 Bodi ya Kudhibiti Kodi za Nyumba imepanga kutekeleza kazi zifuatazo:-

i. Kutoa elimu kwa Taasisi za Serikali na jamii kuhusiana na shughuli, na majukumu ya kisheria ya Bodi ya Kudhibiti Kodi za Nyumba Zanzibar.

ii. Kuongeza ufanisi katika utoaji wa maamuzi ya kesi zinazohusiana na migogoro ya kodi za nyumba kwa kuzitolea maamuzi kesi 35 Unguja na Pemba.

106. Mheshimiwa Spika, ili kuiwezesha Bodi ya Kudhibiti Kodi za Nyumba kutekeleza majukumu yake naliomba Baraza lako kuidhinisha jumla ya **TZS Milioni 94.500** kwa ajili ya utekelezaji wa kazi za kawaida.

BODI YA USAJILI WASANIFU WAHANDISI NA WAKADIRIAJI MAJENGO

107. Mheshimiwa Spika, kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 Bodi ya Usajili Wasanifu Wahandisi na Wakadiraji Majengo imepanga kutekeleza kazi zifuatazo:-

i. Kuendelea na usajili wa Wataalamu 90 wa fani ya ujenzi wa Majengo,Wahitimu, Mafundi Sanifu na Makampuni ya ushauri wa ujenzi kama ilivyoainishwa katika Sheria.

ii. Kuendelea na usajili wa miradi 270 ya ujenzi wa Majengo.

iii. Kuendelea kufanya ukaguzi wa kazi za ujenzi 186 wa majengo zinazofanywa na Wasanifu,Wahandisi na Wakadiriaji Majengo katika maeneo yote ya Unguja na Pemba kwa lengo la kupata ujenzi bora na salama.

iv. Kuendelea kuelimisha Wataalamu wa fani ya Ujenzi kuhusu Ujenzi wa Viwango kwa kufanya Programu 2 za Mafunzo Mafupi .

v. Kuendelea na mpango wa Mafunzo ya Vitendo (Structure Apprentieceship Program) kwa kwawezesha wahitimu wa fani ya Ujenzi kujiunga na Makampuni nchini kwa lengo la kuwapa ujuzi ili waweze kuwa Wataalamu bora.

108. Mheshimiwa Spika, kwa mwaka wa fedha 2023/2024 Bodi ya Usajili Wasanifu Wahandisi na Wakadiraji Majengo imepangiwa kukusanya jumla ya **TZS Milioni 527.00** kutokana na vyanzo vyake mbalimbali vya mapato. Aidha, ili kuiwezesha Bodi ya Usajili Wasanifu Wahandisi na Wakadiraji Majengo kutekeleza majukumu yake kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024, naliomba Baraza lako kuidhinisha jumla ya **TZS Milioni 342.300** kwa ajili ya utekelezaji wa kazi za kawaida.

BODI YA USAJILI WA WAKANDARASI

109. Mheshimiwa Spika, kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 Bodi ya Usajili Wakandarasi imepanga kutekeleza kazi zifuatazo:-

i. Kuendelea na usajili wa Wakandarasi 56 na miradi 220 ya Wakandarasi

ii. Kufanya ukaguzi ili kuhakikisha ujenzi wa miradi 56 unaofanyika Nchini unatekelezwa kwa mujibu wa taratibu na sheria za Bodi ya Usajili wa Wakandarasi na unatimiza viwango vya ujenzi vilivyowekwa.

iii. Kuandaa Semina, Mikutano na mafunzo mbali mbali kwa Wakandarasi, Wajumbe wa Bodi na Watendaji ili kuwajengea uwezo.

iv. Kuwahamasisha wanafunzi kusoma masomo ya Sayansi ili kupata wataalamu wazuri katika fani za ujenzi.

110. Mheshimiwa Spika, kwa mwaka wa fedha 2023/2024 Bodi ya Usajili Wakandarasi imepangiwa kukusanya jumla ya **TZS Bilioni 1.657** kutokana na vyanzo vyake mbalimbali vya mapato. Aidha, ili kuiwezesha Bodi ya Usajili Wakandarasi kutekeleza majukumu yake kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024, naliomba Baraza lako kuidhinisha jumla ya **TZS Milioni 197.120** kwa ajili ya utekelezaji wa kazi za kawaida.

111. Mheshimiwa Spika, kwa mwaka wa fedha 2023/2024 Programu hii imepangiwa kukusanya jumla ya **TZS Bilioni 2.901** kutokana na vyanzo vyake mbalimbali vya mapato.

112. Mheshimiwa Spika, ili kuiwezesha Programu ya Maendeleo ya Makaazi kutekeleza majukumu yake kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024, naliomba Baraza lako kuidhinisha jumla ya **TZS Bilioni 1.275** kwa ajili ya kazi za kawaida ambazo ni ruzuku ya matumizi mengineyo ya Taasisi zilizomo ndani ya program hii.

MUWELEKEO WA BAJETI YA SHIRIKA LA NYUMBA ZANZIBAR

113. Mheshimiwa Spika, kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 Shirika la Nyumba kupitia Programu hii ndogo imepanga kutekeleza kazi zifuatazo:-

i. Kuendelea na ujenzi wa nyumba 72 za Makaazi na biashara Mombasa (kwa Mchina).

ii. Kuendelea na ujenzi wa nyumba 8 za Makaazi na milango ya maduka 11 Mkungu Malofa- ChakeChake.

iii. Kuendelea na mradi wa matengenezo (awamu ya pili) ya nyumba nam. 1699-1705 Mkunazini (Mnadani).

iv. Kuanza kwa matengenezo ya nyumba nam. ZHC 16/06- (Phase I) Kilimatinde, ChakeChake Pemba.

v. Kuanza kwa ujenzi wa Jengo la ghorafa tatu nyumba namba 1299/94 Darajani (kwa Fundi Abduli).

114. Mheshimiwa Spika, Kwa mwaka wa fedha 2023/24 Shirika la Nyumba linatarajia kukusanya jumla ya **TZS Bilioni 13.475** kutokana na kodi zake, mauzo ya nyumba, mikataba, dhamana, na adhabu. Pamoja na mapato yanayotarajiwa kupatikana kwa kazi za ujenzi na ushauri elekezi za kampuni ya Shirika. Hata hivyo Shirika linatarajia kuchukuwa mkopo kutoka katika taasisi za kifedha kwa ajili ya kuongeza mfuko wa ujenzi wa nyumba unaotarajiwa kujengwa Mombasa kwa Mchina.

115. Mheshimiwa Spika, Kwa upande wa Matumizi Shiriki la Nyumba Kwa mwaka wa fedha 2023/24 Shirika limekadiria kutumia jumla ya **TZS Bilioni 13.246** kwa kazi za kawaida na kazi za Maendeleo.

SHUKURANI

116. Mheshimiwa Spika, naomba kuchukua fursa hii kwa mara nyengine tena kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijaalia fursa, uwezo wa kuisoma hotuba hii ya bajeti ya Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi kwa mwaka wa fedha 2023/2024.

117. Mheshimiwa Spika, naomba uniruhusu kumshukuru tena Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Hussein Ali Mwinyi, kwa imani yake tena kwangu na kunipa nafasi hii muhimu ya kuitumikia Nchi yangu kupitia Wizara hii, nami naahidi nitajitahidi kadri ya uwezo wangu wote kumsaidia. Aidha, namshukuru Mheshimiwa Makamo wa Kwanza wa Rais na Makamo wa Pili wa Rais kwa maelekezo yao wanayonipatia. Wote nawaombea kwa Mwenyezi Mungu awazidishie busara, uadilifu, afya njema na maisha marefu pamoja na familia zao.

118. Mheshimiwa Spika, kwa mara nyengine tena naomba kukushukuru wewe mwenyewe, Naibu Spika na Waheshimiwa wote kwa kunisikiliza kwa utulivu na kwa umakini mkubwa wakati nikisoma hotuba ya Wizara yangu.

119. Mheshimiwa Spika, naomba pia kuwashukuru Wenyeviti na Wajumbe wa Kamati za Kudumu za Baraza la Wawakilishi zilizotembelea na kufanya vikao na Wizara hii. Maoni, ushauri na maelekezo yao kwetu yamesaidia sana sio tu katika utekelezaji wa kazi za Wizara bali pia katika utayarishaji wa Hotuba hii. Shukurani maalumu kwa Kamati ya Mawasiliano, Ardhi na Nishati kwa msaada na Ushirikiano wao mkubwa waliotupatia.

120. **Mheshimiwa Spika,** shukurani maalumu ziwaendee wafanyakazi wa Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi Unguja na Pemba kwa Ushirikiano wao mkubwa kwangu, namuomba Mwenyezi Mungu awajaalie wote afya njema na maisha marefu yenye kheri. Naamini ushirikiano huo utaendelea ili tuweze kuendelea kutoa huduma bora kwa Wananchi.

121. **Mheshimiwa Spika,** Kipekee naomba niushukuru Ungozi wa Wizara hususan Mheshimiwa Juma Makungu Juma, Naibu Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makaazi, Katibu Mkuu Dkt Mngereza Mzee Miraji Naibu Katibu Mkuu ndugu, Mzee Ali Haji, Afisa Mdhamini Ndugu, Bakari Ali Bakari Wakurugenzi, Wakuu wa Taasisi na Wafanyakazi wote kwa kuwa na mimi bega kwa bega katika kuhakikisha Wizara inatekeleza majukumu yake kulingana na matakwa ya nchi na kuwapatia wananchi maendeleo pamoja na huduma zilizokuwa bora Zaidi.

122. **Mheshimiwa Spika,** pia nachukua fursa hii kuwashukuru Wadau mbalimbali wa Serikali na wasio wa Serikali wakiwemo Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Idara Maalamu za SMZ, Ofisi ya Rais Fedha na Mipango, Wizara ya Ujenzi Mawasiliano na Uchukuzi, Wizara Kilimo Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo, Wizara ya Maji, Nishati na Madini, Wakuu wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya, Mamlaka ya Serikali za Mitaa (LGAs), Kikosi cha kuzuia Magendo KMKM, ZIPA, Mamlaka ya Mapato Zanzibar (ZRA), Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, MKURABITA, Masheha pamoja na Wananchi wote kwa ushirikiano mkubwa kwa Wizara yangu kwa kuhakikisha kuwa majukumu tuliopewa yanatekelezwa kama yalivyokusudiwa na kwa ufanisi mkubwa.

123. **Mheshimiwa Spika,** na kwa mwaka ujao wa Fedha 2023/2024, Wananchi wategemee ongezeko kubwa la ubora wa huduma na ufanisi katika utendaji wa kazi za Wizara, licha ya changamoto kubwa ya migogoro ya ardhi ya muda mrefu inayoendelea, uwepo wa ujenzi holela usiofuata mipango miji pamoja na kuwepo kwa kiu kubwa kwa jamii ya kuwa na Makaazi bora, nafuu na salama. Wizara itahakikisha usimamizi wa ardhi, utatuzi wa migogoro ya ardhi na udhibiti wa ujenzi utaimarika zaidi kutokana na mikakati iliyowekwa sambamba na kuimarisha Miji yetu kwa ujenzi wa nyumba za kisasa ambazo ni za bei nafuu.

124. **Mheshimiwa Spika,** kwa namna ya pekee, napenda kuishukuru familia yangu kwa ustahamilivu, subra na ushirikiano mkubwa wanaonipatia katika kutekeleza majukumu niliokabidhiwa. Na kwa upekee nawashukuru Kinamama wa Mkoa wa Kusini Unguja kwa ushirikiano wao wa dhati wanaonipatia katika kutekeleza shughuli mbalimbali za Jumuiya yetu.

MAOMBI YA FEDHA KWA MWAKA 2023/2024

125. **Mheshimiwa Spika,** ili Wizara yangu iweze kutekeleza Programu Kuu na Programu Ndogo nilizozieleza, naiomba Kamati yako iidhinishe jumla ya fedha **TZS 17,009,200,000** kwa utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi kwa mwaka wa fedha 2023/2024 kati ya hizo **TZS 7,023,900,000** kwa kazi za kawaida, mishahara na ruzuku kwa Taasisi zilizochini ya fungu la Wizara. Aidha Jumla ya **TZS 5,435,300,000** kwa kazi za kawaida, mishahara na ruzuku pamoja na **TZS 4,550,000,000** kwa kazi za Maendeleo kwa ajili ya fungu la Kamisheni ya Ardhi.

126. Mheshimiwa Spika, pia naomba idhini ya kukusanya Mapato ya Fedha **TZS 7,505,605,000** kutoka vyanzo mbalimbali vya Wizara yangu, ambapo **TZS 4,754,713,000** kutoka katika vianzio mbali mbali vilivyomo ndani ya fungu la Wizara, na **TZS 2,750,892,000** kwa ajili ya Mapato yanayotokana na vianzio mbali mbali vilivyomo ndani la Fungu la Kamisheni ya Ardhi. Kwa ufafanuzi zaidi naomba angalia **kiambatisho "D1, D2, D3 na D4".**

HITIMISHO

127. Mheshimiwa Spika, nawaomba sasa Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako waipokee, waijadili kwa kina, kisha watushauri na kutuelekeza na hatimae wayapitishe makadirio haya. Tuna imani kubwa kuwa michango ya waheshimiwa wajumbe itatusaidia sana katika kutekeleza majukumu yetu ya kazi vizuri zaidi katika kipindi kijacho cha Mwaka wa Fedha 2023/2024.

128. Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

Mheshimiwa Rahma Kassim Ali (MBM)
Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makaazi Zanzibar.

VIAMBATISHO

KIAMBATANISHO “A1”

MAFUNZO YA MUDA MFUPI KWA WAFANYAKAZI WA WIZARA YA ARDHI NA MAENDELEO YA MAKAAZI KWA MWAKA WA FEDHA 2022/2023

S/N	TAASISI	M'ME		W'KE		JUMLA
		NDANI YA NCHI	NJE YA NCHI	NDANI YA NCHI	NJE YA NCHI	
1	UTUMISHI NA UENDESHAJI	3	-	4	-	7
3	WAKALA WA MAJENGO	2	-	7	-	9
4	MAHAKAMA YA ARDHI	1	-	3	-	4
5	SHIRIKA LA NYUMBA	10	-	-	-	10
6	BODI YA KONDOMINIO	1	-	2		3
7	MTHAMINI MKUU	3	-	5	-	8
8	KAMISHENI YA ARDHI	5	-	11	-	16
	JUMLA KUU	**25**		**32**		**57**

KIAMBATANISHO NAMBARI "A2"

MAFUNZO YA MUDA MREFU KWA WAFANYAKAZI WA WIZARA YA ARDHI NA MAENDELEO YA MAKAAZI 2022/2023

TAASISI	AINA YA MAFUNZO	W'ME	W'KE	JUMLA	CHUO	MWAKA WA KUMALIZA
IDARA YA UTUMISHI NA UENDESHAJI	DEGREE IN MASS COMMUNICATION	-		1	OPEN UNIVERSITY	2025
	DEGREE RECORD AND ACHIEVE MANAGEMENT	1		1	INSTITUTE OF PUBLIC ADMINISTRATION	2023
	MASTER IN BUSINESS ADMINISTRATION	-	1	1	UNIVERTY OF DAR ES SALAM	2024
	MASTER IN DATA SCIENCE	1	1	2	UNIVERTY OF DAR ES SALAM	2024
	DEGREE IN DATA SCIENCE	1	-	1	UNIVERTY OF DAR ES SALAM	2025
	MASTER OF LAW	-	1	1	OPEN UNIVERSTY	2025
IDARA YA MIPANGO SERA NA UTAFITI	MASTER OF RESEARCH AND PUBLIC POLICY		1	1	CHUO CHA MIPANGO DODOMA	2023
AFISI KUU PEMBA	DEGREE IN HUMAN RESOURCE MGNT		1	1	INSTITUTE OF PUBLIC ADMINISTRATION	2024
	DIPLOMA IN RECORDING AND ARCHIVE MANAGEMENT		2	2	INSTITUTE OF PROFFESIONAL AND INNOVATION DEVELOPMET	2024
	DIPLOMA IN ECONOMY DEVELOPMENT		1	1	MWALIMU NYERERE MOMORIAL ACADEMY	2024

	MASTER IN BUSENESS ADMINISTRATION		1	1	BEJIN INTERNATIONAL STUDIES UNIVERSITY	2024
WAKALA WA MAJENGO	DEGREE IN BUSINES ADMINISTRATION		1	1	KAMPALA INTERNATIONA UNIVERSITY	2024
	MASTER OF CIVIL ENGINNERING		1	1	UNIVERSITY OF DERESALAM	2024
	MASTER IN ARCHITECTURE	-	1	1	CYPRUS UNIVERSITY	2024
	DIPLOMA IN INTERNATIONAL RELATION	1	-	1	IPA	2024
	CERTIFICATE IN BUSSINESS ADMINISTRATION IN LEARDERSHIP AND GOOD GERVERNANCE	1	-	1	ZANZIBAR UNIVERSITY	2024
WAKALA WA MAJENGO - PEMBA	DEGREE IN QUANTITY SURVEY	2		2	ARDHI UNIVERSITY	2025
	MASTER IN TRANSPORT AND LOGISTIC MANAGEMENT		1	1	OPEN UNIVERSITY	2024
	DIPLOMA IN PUBLIC ADMINISTRATION	1	-	1	INSTITUTE OF PUBLIC ADMINISTRATION	2024
MAHAKAMA YA ARDHI	DEGREE IN LAW		1	1	ZANZIBAR UNIVERSITY	2024
BODI YA KONDOMINIO	CERTERFIFICATE RECORD AND ACHIEVE MANAGEMENT	1	-	1	ICPS - ZANZIBAR	2024

SHIRIKA LA NYUMBA	PHD IN ECONOMICS	1	0	1	POLTOVA UNIVERSITY OF ECONOMICS (UKRAINE)	2022
	DEGREE IN ARCHITECTURE	0	1	1	ARDHI UNIVERSITY	2026
	CERTIFICATE IN ELECTRIC ENGINEERING	1	0	1	TAASISI YA KARUME YA SAYANSI NA TEKNOLOJIA	2022
MTHAMINI MKUU WA SERIKALI	MSc, REAL ESTATE BUSINESS		1	1	ARDHI UNIVERSITY	2022
KAMISHENI YA ARDHI	DEGREE OF INVEROMENTAL PLANNING AND MANAGEMENT	1		1	INSTITUTE OF RURAL DEVELOPMENT PLANNING	2023
	HUMAN RESOURCE MANAGEMENT		1	1	DODOMA	2022
	ENVIRONMENTAL PLANNING	1		1	DODOMA	2023
	CIVIL ENGENER	1		1	BUDAPEST HANGRY	2022
	RECOD AND ARCHIVE MENAGEMENT		1	1	IPA	2023
	URBAN PLANNING		1	1	UNIVERSITY OF DERESALAM	2022
	MANAGEMENT AND SOCIAL DEVELOPMENT	1		1	MWALIM NYERERE - ZNZ	2023
	MECHANICAL ENGENEARING	1		1	KARUME INSTITUTE	2022
	PHD IN DESIGN AND ARCHITECTURE	1	-	1	ALTO UNIVERSITY - FINLAND	2025
KAMISHENI YA ARDHI - PEMBA	MASTER OF LOW IN LAND	1		1	OPEN UNIVERSITY	2025

	ADMINISTRATION AND MANAGEMENT					
	DEGREE IN LAND MANAGEMENT AND VALUATION	1		1	ARDHI UNIVERSITY	2024
	DEGREE IN URBAN PLANNING	1		1	ARDHI UNIVERSTY	2024
	DEGREE IN MASS COMMUNICATION	1		1	OPEN UNIVERSITY	2024

KIAMBATANISHO NAMBARI "B1"

MUHTASARI WA UKUSANYAJI WA MAPATO KWA KIPINDI CHA JULAI 2022 - MACHI 2023.

TAASISI	KASMA	CHANZO CHA MAPATO	FEDHA ILIYOPANGWA KUKUSANYWA KWA MWAKA	FEDHA ILIYOKUSANYWA JULAI 2022 – MACHI 2023	ASILIMIA YA FEDHA ILIYOKUSANYWA
AFISI KUU PEMBA	1422008	Ukodishwaji wa Mashine	1,000,000	513,000	51.3
	1422070	Fii ya Korti	7,000,000	3,003,399	43
	1415003	Kodi ya Majengo ya Serikali	10,000,000	3,803,500	38
	1430009	Adaya ya ushauri	79,000,000	2,029,750	3
	Jumla ndogo		**97,000,000**	**9,349,649**	**10**
DEVELOPMENT CONTROL UNIT (DCU)		Ada ya Vibali vya Ujenzi	918,000,000	381,532,700	42
	Jumla ndogo		**918,000,000**	**381,532,700**	**42**
KAMISHENI YA ARDHI	1422008	Nyaraka za Ardhi	393,784,000	380,642,281	97
	1422028	Muongozo wa matumizi ya ardhi	49,095,000	62,219,372	127
	1422043	Upimaji na Ramani	430,605,000	544,867,701.50	127
	1422074	Usajili wa Ardhi	73,642,000	39,497,000	54

	1422093	Uthamini	75,688,000	43,888,840	58
	1422090	Uhaulishaji	-	554,967,520	
	Jumla ndogo		**1,022,814,000**	**1,626,082,714.50**	**159**
MAHAKAMA YA ARDHI	1422072	Fii ya Korti	10,000,000	7,779,001	76
	Jumla ndogo		**10,000,000**	**7,779,001**	**76**
OFISI YA MTHAMINI MKUU WA SERIKALI	1422093	Ada ya Uthamini	250,000,000	219,060,000	88
	Jumla ndogo		**250,000,000**	**219,060,000**	**88**
BODI YA KONDOMINIO	1422119	Ada ya usajili wa Kondominio	325,000,000	249,869,498	76
	Jumla ndogo		**325,000,000**	**249,869,498**	**77**
WAKALA WA MAJENGO	1415011	Ukodishwaji wa mashine	3,000,000	0	0
	1422077	Mapato ya Kazi za Biashara	35,000,000	1,800,000	5
	1430009	Ada ya ushauri elekezi	240,000,000	83,550,000	35
	1415003	Ukodishwaji wa Majengo ya Serikali	22,000,000	18,613,000	85
	Jumla ndogo		**300,000,000**	**103,963,000**	35
	JUMLA KUU		**2,922,815,000**	**2,597,636,562.5**	**89**

KIAMBATANISHO “C1”

MUHUTASARI WA MATUMIZI YA PROGRAMU KUU NA PROGRAMU NDOGO KWA KIPINDI CHA JULAI 2022 – MACHI 2023 IKILINGANISHWA KWA MAKADIRIO YA MWAKA

PROGRAMU KUU	IDARA/ TAASISI	MAKISIO KWA MWAKA	MISHAHARA NA POSHO	MATUMIZI MENGINEYO NA MAENDELEO	JUMLA YA FEDHA ZILIZOPATIKANA KWA MIEZI 9	%	MISHAHARA NA POSHO	%	MATUMIZI MENGINEYO NA MAENDELEEO	%
Uendeshaji na Uratibu wa Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi	Idara ya Mipango Sera na Utafiti	335,270,000	151,270,000	184,000,000	194,367,020	**58**	123,367,020	**82**	70,781,680	**38**
	Idara ya Uendeshaji na Utumishi	2,074,800,000	1,583,800,000	491,000,000	2,109,110,192	**102**	1,901,405,460	**118**	207,704,732	**42**
	Ofisi Kuu Pemba	747,600,000	565,600,000	182,000,000	658,410,425	**88**	586,968,425	**104**	71,442,000	**39**
	Jumla ndogo	**3,157,670,000**	**2,300,670,000**	**857,000,000**	**2,961,887,637**	**93**	**2,611,740,905**	**114**	**349,928,412**	**39**
Usimamizi wa Ardhi	Mahakama ya Ardhi	584,000,000	258,000,000	326,000,000	297,581,718	**58**	241,492,330	**94**	56,089,388	**17**
	Afisi ya Mthamini Mkuu wa Serikali	162,400,000	-	162,400,000	42,800,000	**26**	-	-	42,800,000	**26**
	Mradi wa Mpango wa Matumizi ya Ardhi	1,000,000,000	-	1,000,000,000	-	**0**	-	**0**	-	**0**
	Jumla ndogo	**1,746,400,000**	**258,000,000**	**1,488,400,000**	**340,381,718**	**19**	**241,492,330**	**94**	**98,889,388**	**7**
	Kamisheni ya Ardhi	4,216,600,000	1,785,098,900	2,431,500,258	2,631,416,110	**62**	2,116,979,710	**119**	514,484,400	**21**
	Jumla ndogo ya Programu	**5,963,000,000**	**2,043,098,900**	**3,919,900,258**	**2,971,797,828**	**50**	**2,358,472,040**	**115**	**613,373,788**	**16**
Maendeleo ya Makaazi	Bodi ya Kudhibiti Kodi za Nyumba	135,000,000	-	135,000,000	36,600,000	27	-	-	36,600,000	27
	Bodi ya Kondominio	240,000,000	-	240,000,000	173,860,000	72	-	-	173,660,000	72
	Bodi ya Usajili Wahandisi, Wasanifu na Wakadiriaji Majengo	676,000,000	-	676,000,000	81,025,600	12	-	-	81,025,600	12

	Bodi ya Usajili Wakandarasi	281,600,000	-	281,600,000	71,053,800	25	-	-	71,053,800	25
	Wakala wa Majengo	489,000,000	-	489,000,000	301,433,469	62	-	-	301,433,469	62
	Jumla Ndogo	**1,821,600,000**	**-**	**1,821,600,000**	**663,972,869**	**36**	**-**	**-**	**663,972,869**	**36**
	Mradi wa ukarabati wa nyumba za Maendeleo	16,000,000,000	-	16,000,000,000	0	0	-	-	0	**0**
	Jumla ndogo	**17,821,600,000**	**-**	**17,821,600,000**	**663,972,869**	**4**			**663,972,869**	**4**
	JUMLA KUU	**26,942,270,000**	**4,343,768,000**	**22,598,500,258**	**6,597,658,334**	**24**	**4,970,212,945**	**114**	**1,672,275,814**	**7**

KIAMBATANISHO "D1"

MAKADIRIO YA FEDHA ZA MATUMIZI KWA FUNGU LA WIZARA KWA MWAKA WA FEDHA 2023/2024

Na.	PROGRAMU	PROGRAMU NDOGO	TAASISI/IDARA	MAKISIO KWA MWAKA 23/24				
				MATUMIZI MENGINEYO	MISHAHARA	RUZUKU	KAZI ZA MEANDELEO	JUMLA YA FEDHA ILIYOPANGWA
1	1. Uendeshaji na Uratibu wa Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi	1. Uratibu wa Mipango, Sera na Utafiti	Idara ya Mipango Sera na Utafiti	557,018,000	187,412,000	-	-	744,430,00
		2. Utawala na Uendeshaji	Idara ya Uendeshaji na Utumishi	405,001.000	2,744,061,000	-	-	3,149,062,00
		3. Uratibu na utekelezaji wa shuhuli za Wizara Pemba	Afisi Kuu Pemba	248,581,000	805,423,000	-	-	1,054,004,00
		Jumla ndogo		**1,210,600,000**	**3,736,896,000**	**-**	**-**	**4,947,496,11**
	2. Usimamizi wa Ardhi	1. Usimamizi wa Ardhi	Afisi ya Mthamini Mkuu wa Serikali	-	-	213,680,000	-	213,680,00
			Mahakama ya Ardhi	245,000,000	342,604,000	-	-	587,604,00
		Jumla Ndogo		**245,000,000**	**342,604,000**	**213,068,000**		**801,284,00**
	3. Maendeleo ya Makaazi	1. Maendeleo ya Makaazi	Wakala wa Majengo	-	-	473,200,000		473,200,00
			Bodi ya Kondominio	-	-	168,000,000	-	168,000,00
			Bodi ya Kudhibiti Kodi za Nyumba	-	-	94,500,000	-	94,500,00
			Bodi ya Usajili Wasanifu, Wahandisi na Wakadiriaji Majengo	-	-	342,300,000	-	342,300,00

			Bodi ya Usajili Wakandarasi	-	-	197,120,000	-	
			Jumla ndogo	**-**	**-**	**1,275,120,000**	**-**	**1,275,120,00**
			JUMLA KUU	**1,455,600,000**	**4,079,500,000**	**1,488,188,000**	**-**	**7,023,288,00**

KIAMBATANISHO “D2”

MAKADIRIO YA UKUSANYAJI WA MAPATO KWA FUNGU LA WIZARA KWA MWAKA WA FEDHA 2023/2024

TAASISI	KASMA	CHANZO CHA MAPATO	FEDHA ILIYOPANGWA KUKUSANYWA
OFISI KUU PEMBA	1422016	Ada ya Vibali vya Ujenzi (DCU)	21,000,000
	1422070	Fii ya Korti	7,000,000
	1415003	Ukodishwaji wa Majengo ya Serikali	10,000,000
	1430009	Ada ya ushauri elekezi	60,000,000
	Jumla ndogo		**98,000,000**
WAKALA WA MAJENGO	1422077	Mapato ya Kazi za Biashara	35,000,000
	1430009	Ada ya ushauri elekezi	309,000,000
	1415003	Ukodishwaji wa Majengo ya Serikali	22,000,000
	Jumla ndogo		**366,000,000**
MAHKAMA YA ARDHI	1422072	Fii ya Korti	10,000,000
	Jumla ndogo		**10,000,000**
MTHAMINI WA ARDHI	1422093	Ada ya Uthamini	270,000,000
	Jumla ndogo		**270,000,000**
BODI YA KONDOMINIO	1422119	Ada ya usajili wa Kondominio	350,000,000
	Jumla ndogo		**350,000,000**
IDARA YA MIPANGO	1422016	Ada ya Vibali vya Ujenzi (DCU)	1,476,000,000
	Jumla ndogo		**1,476,000,000**
BODI YA USAJILI WA WAKANDARASI	**1500009**	Mapato yatokanayo na Bodi ya Wakandarasi	1,567,713,000
	Jumla ndogo		**1,657,713,000**
BODI YA USAJILI WASANIFU, WAHANDISI NA WAKADIRIAJI MAJENGO	**1112006**	Mapato yatokanayo na Bodi ya AEQSRB	**527,000,000**
	Jumla ndogo		**527,000,000**
		JUMLA KUU	**4,754,713,000**

KIAMBATANISHO "D3"

MAKADIRIO YA FEDHA ZA MATUMIZI KWA KAZI ZA KAWAIDA NA MAENDELEO KWA KAMISHENI YA ARDHI KWA MWAKA WA FEDHA 2023/2024

No.	PROGRAMU	PROGRAMU NDOGO	TAASISI/IDARA		MAKISIO KWA MWAKA			
				MATUMIZI MENGINEYO	MISHAHARA	RUZUKU	KAZI ZA MAENDELEO	JUMLA YA FEDHA ILIYOPANGWA
1	Utawala na Uendeshaji wa Kamisheni ya Ardhi	1. Uratibu wa shughuli za Utawala na Mipango	Afisi ya Katibu Mtendaji	389,069,000	2,287,472,000	-	-	2,676,541,00
		2. Uratibu wa shughuli za Afisi ya Katibu Mtendaji		6,395,000	-	-	-	6,395,00
		3. Uratibu wa shughuli za Kamisheni Pemba	Afisi ya Uratibu Pemba	572,869,000	753,252,000	-	-	1,326,121,00
		Jumla ndogo		**968,333,000**	**3,040,724,000**	**-**	**-**	**4,009,057,00**
2	Utawala na Usimamizi wa Ardhi	1. Ugawaji na Usimamizi wa Ardhi	Idara ya Ardhi na Uhaulishaji wa Ardhi	313,632,040	-	773,075,960	-	1,086,708,00
		2. Upimaji na utayarishaji wa Ramani	Idara ya Upimaji na Ramani	144,918,000	-	-	-	144,918,00
		3. Usajili wa Ardhi	Afisi ya Mrajis wa Ardhi	128,050,000	-	-	-	128,050,00
		4. Uandaaji wa mipango ya matumizi Ardhi Mijini na Vijijini	Idara ya Mipango Miji na Vijiji	66,567,000	-	-	4,550,000,000	4,616,567,00
		Jumla ndogo		**653,167,040**		**773,075,960**	**4,550,000,000**	**5,976,243,00**
		JUMLA KUU		**1,621,500,040**	**3,040,724,000**	**773,075,960**	**4,550,000,000**	**9,985,300,00**

KIAMBATANISHO “D4”

MAKADIRIO YA MAKUSANYO WA MAPATO KWA KAMISHENI YA ARDHI KWA MWAKA WA FEDHA 2023/2024

TAASISI	KASMA	CHANZO CHA MAPATO	FEDHA ILIYOPANGWA KUKUSANYWA
KAMISHENI YA ARDHI	**1422093**	Ada ya Uthamini	**92,555,871**
	1422028	Muongozo wa Matumizi ya Ardhi	**60,041,529**
	1422008	Nyaraka za Ardhi	**481,584,548**
	1422043	Ada ya Upimaji na Ramani	**526,615,387**
	1422072	Ada ya Usajili wa Ardhi	**90,094,665**
	1422090	Uhalishaji wa Arddhi	**1,500,000,000**
	JUMLA KUU		**2,750,892,000**

KIAMBATANISHO E1:

KAZI ZA USHAURI ELEKEZI ZILIZOTEKELEZWA NA ZBA KWA KIPINDI CHA ROBO TATU (JULAI- MACHI, 2023).

No.	AINA YA KAZI NA AFISA / MAOFISA WANAOSIMAMIA.	MTOA KAZI	MAJUKUMU YA ZBA	MAHALA PA KAZI	MAELEZO YA UTEKELEZAJI.
1.	Ujenzi wa Kituo cha Kurekebisha Tabia	Mamlaka ya Udhibiti wa Matumizi ya Dawa za Kulevya	Kusimamia Ujenzi	KIDIMNI	Wakala inaendelea na usimamizi wa ujenzi
2.	Matayarisho ya Nyaraka za Ujenzi kwa Kazi ya Ujenzi wa Afisi na Maabara ya Dawa na Chakula	ZFDA.	Kutayarisha Ramani, BoQ na Nyaraka za Zabuni	CHAMANANGWE-PEMBA	Wakala imeshakamilisha kazi hiyo na kuikabidhi kwa wahusika
3.	Uandaaji wa Michoro na BoQ kwa ujenzi wa ofisi ya Uhamiaji Mkoa wa Mjini Magharibi.	Idara ya Uhamiaji	Kutayarisha Ramani na BoQ	MAZIZINI, ZANZIBAR	Michoro imeshawasilishwa kwa wahusika.
4.	Uandaaji wa Michoro na BoQ kwa ujenzi wa nyumba za Idara ya Uhamiaji Chukwani –Zanzibar	Idara ya Uhamiaji	Kutayarisha Ramani na BoQ	CHUKWANI, ZANZIBAR	Michoro imeshawasilishwa kwa wahusika.
5.	Kuandaa michoro na BoQ kwa ujenzi wa kituo cha Maendeleo ya Vijana vitakavyojengwa Muyuni-Unguja na Mbuzini-Pemba.	Wizari ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo	Kutayarisha Ramani, BoQ na Nyaraka za Zabuni	MUYUNI-UNGUJA NA MBUZINI-PEMBA.	Kazi ya kuandaa michoro hiyo inaendelea
6.	Usimamizi wa Ujenzi wa Kiwanda cha Mwani Chamanagwe.	Kampuni ya Mwani	Usimamizi wa mradi	CHAMANANGWE-PEMBA	Kazi ya usimamizi wa mradi unaendelea.
7.	Kuandaa michoro ya Ukuta (fence wall) wa eneo la maonyesho ya biashara	Wizara Biashara na Maendeleo ya Viwanda.	Kutayarisha Ramani, BoQ na Nyaraka za Zabuni	NYAMANZI, ZANZIBAR	Utayarishaji wa Ramani na BoQ umekamilika na kuwasilishwa kwa client.

8.	Kuandaa michoro na BoQ ya ujenzi wa ghorofa ya juu ya Ofisi ya DPP.	Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka.	Kutayarisha Ramani na BoQ Pamoja na Usimamizi wa Mradi	MIEMBENI-ZANZIBAR	Utayarishaji wa Ramani na BoQ umekamilika na kuwasilishwa kwa wahusika.
9.	Usimamizi wa ujenzi wa Soko la Mwanakwerekwe	Manispaa ya Magharibi B	Usimamizi wa Ujenzi	MWANAKWEREKWE	Usimamizi wa ujenzi unaendelea
10.	Usimamizi wa ujenzi wa Soko la Jumbi	Manispaa ya Magharibi B	Usimamizi wa Ujenzi	JUMBI	Usimamizi wa ujenzi unaendelea
11.	Usimamizi wa ujenzi wa Soko la Chuini	Manispaa ya Magharibi A	Usimamizi wa Ujenzi	CHUINI	Usimamizi wa ujenzi unaendelea
12.	Uandaaji wa Michoro ya ujenzi wa Landscape ya ofisi Idara ya Ushirika.	Afisi ya Rais Kazi, Uchumi na Uwekezaji.	Kutayarisha Ramani, BoQ na Nyaraka za Zabuni, Pamoja na Usimamizi wa mradi	MIGOMBANI-ZANZIBAR.	Utayarishaji wa Ramani na BoQ umeshakamilika.
13	Ushauri Elekezi katika kazi ya kuandaa michoro ya partition za ofisi.	Bodi ya Mkopo Elimu ya juu.	Pre-Contract (Kutayarisha Ramani, BoQ na Nyaraka za Zabuni	JENGO LA SHOPPING MALL-ZANZIBAR	Utayarishaji wa Ramani na BoQ umekamilika na tayari ramani zimeshawasilishwa kwa mteja,malipo bado hayajafanyika.
14	Ushauri Elekezi katika kazi ya kupitia michoro na usimamizi wa vituo vitano vya amali pamoja jengo la Karume Institute of Science and Technology.	Wizara ya Elimu na vituo vya Amali.	Review of Design and Post -Contract (Kutayarisha Ramani, BoQ na Nyaraka za Zabuni pamoja na usimamizi wa mradi.	MBWENI-ZANZIBAR Vitano Unguja Vitatu Pemba	Technical and Financial Proposal imeshawasilishwa kwa Mmiliki wa mradi.
15	Kupatiwa Ushauri wa ujenzi wa PAA katika jengo la Zura.	Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati Zanzibar	Pre-Contract (Kutayarisha Ramani, BoQ.	MAISARA-ZANZIBAR	Michoro pamoja na BoQ zimeshawasilishwa kwa Client.

16	Kuandaa mchoro wa ukarabati wa jengo sambamba na kusimamia ukarabati wa jengo la Afisi ya Shirika la Meli iliopo Malindi Unguja katika makao makuu ya Shirika na Afisi ndogo ya Da res Salaam.	Shirika la Meli-ZANZIBAR	Pre-Contract (Kutayarisha Ramani, BoQ.	UNGUJA-ZANZIBAR NA DAR ES SALAAM.	Michoro pamoja na BoQ zinatayarishwa.
17	Kutayarisha Gharama za kuboresha ukumbi wa ZEMA.	ZEMA	Pre-Contract (Kutayarisha Ramani, BoQ.	MARUHUBI-ZANZIBAR	Michoro pamoja na BoQ zimeshawasilishwa kwa Client.
18	Kutayarisha Gharama za kuboresha vyumba vya maabara ya vimelea na kemia	TAASISI YA UTAFITI WA UVUVI NA MALIASILI ZA BAHARINI	Pre-Contract (Kutayarisha Ramani, BoQ.	MARUHUBI-ZANZIBAR	Michoro pamoja na BoQ zimeshawasilishwa kwa Client.

KIAMBATISHO E2:

UTEKELEZAJI ROBO TATU USIMAMIZI WA NYUMBA JULAI – MACHI, 2023)

Na.	AINA YA KAZI	MALENGO KWA NUSU MWAKA	ROBO YA KWANZA	ROBO YA PILI	ROBO YA TATU	MAELEZO YA UTEKELEZAJI
1.	Ukusanyaji wa Mapato ya Serikali yatokanayo na Kodi za Nyumba na Ada za Majengo zinazosimamiwa na Wakala wa Majengo Zanzibar.	Kukusanya Kodi za Nyumba kiasi cha Shilingi Millioni Ishirini na Tano, Laki Mbili na Elfu Ishirini na Tano **(TShs 25,225,000/=)**	Kukumbushia na kufuatilia malipo ya kodi ya nyumba na Ada za Majengo kwa wapangaji. Jumla ya Shilingi **Milioni Sita na Laki tisa 6,900,000/=** zimekusanywa.	Kukumbushia na kufuatilia malipo ya kodi ya nyumba na Ada za Majengo kwa wapangaji Jumla ya Shilingi **Milioni Sita na Laki Mbili (6,200,000/=)** zimekusanywa	Kukumbushia na kufuatilia malipo ya kodi za Nyumba na Ada za Majengo kwa wapangaji Jumla ya Shilingi **Milioni Nne, Laki Sita na Elfu Tisiini (4,690,000/=)** zimekusanywa.	Wakala wa Majengo ilikukusanya Kodi za nyumba na Ada za majengo kiasi cha **Shilingi Milioni Kumi na Saba Laki Saba na Elfu Tisiini (TShs 17,790,000/=)**
2.	Ukaguzi na uhakiki **''inspection and inventory''** wa Nyumba za Wakala wa Majengo.	Kupata taarifa ya hali halisi ya Majengo na wakaazi wake.	Ukaguzi na uhakiki wa Nyumba No S-51, S-50 na 42/101/P3	Ukaguzi na uhakiki wa nyumba N0 SH/KS/49M, SH/KS/50M na SH/KS/52M Mazizini	Ukaguzi na uhakiki wa nyumba N0 SH/KS/53M, SH/KS/54M na SH/KS/55M Mazizini	Jumla ya Nyumba 9 zilikaguliwa na kufanyiwa uhakiki pamoja kuandaa ripoti ya ukaguzi huo.
3.	Kuzitia thamani Nyumba zinazomilikiwa na wakala wa majengo.	Kutambua thamani halisi (Market value) ya Nyumba N0 S-51, S-50, 42/101/P3, SH/KS/49M, SH/KS/50M, SH/KS/52M SH/KS/53M, SH/KS/54M, SH/KS/55 za	Ukaguzi wa Nyumba 3 pamoja na kuandaa ripoti ya Tathmini ya Nyumba No S-51, S-50 na 42/101/P3	Ukaguzi wa Nyumba 3 pamoja na kuandaa ripoti ya Tathmini ya Nyumba N0 SH/KS/49M, SH/KS/50M na SH/KS/52M Mazizini	Ukaguzi wa Nyumba 3 pamoja na kuandaa ripoti ya Tathmini ya Nyumba No SH/KS/53M, SH/KS/54M na SH/KS/55M Mazizini	Jumla ya Nyumba 9 zilifanyiwa tathimini na kuandaliwa ripoti zake.

		Wakala wa Majengo.				
4.	Uandaaji wa Mikataba Mipya ya ukodishwaji wa nyumba na majengo ya biashara	Kutoa mikataba mipya kwa wakodishwaji waliomaliza muda wao.	Upitiaji na utayarishaji wa mikataba mipya umefanyika	Upitiaji na utayarishaji wa mikataba mipya umefanyika	Upitiaji na utayarishaji wa mikataba mipya umefanyika	Mikataba ilipitiwa na kutayarishwa.inasubiriwa miongozo ya Serikali
5.	Kufuatilia upatikanaji wa hati milki za Nyumba/Majengo .	Kupata umiliki wa nyumba zinazomilikiwa na wakala wa majengo	Maombi ya kupatiwa hati za majengo yaliwasilishwa COLA	Tunasubiri hatua za utekelezaji kutoka COLA	Tunasubiri hatua za utekelezaji kutoka COLA	Utekelezaji bado haujafanyika. ZBA haijapokea gharama za malipo ya kazi hiyo.
6.	Uandaaji wa wazo la Mradi wa Ujenzi Nyumba Mpya za Watumishi wa Umma ..	Kupata Majengo matano yaa ghorofa tano kila moja (G+5) kwa ajili makaazi ya watumishi wa umma.	Utayarishaji wa Ramani pamoja na BOQ unaendelea	Utayarishaji wa Ramani pamoja na BOQ unaendelea	Utayarishaji wa Ramani pamoja na BOQ unaendelea	Ukamilishaji wa Ramani pamoja na BOQ ili ziwasilishwe wizarani

KIAMBATISHO F1:

MAENEO YENYE MIGOGORO YA ARDHI YALIYOFUATILIWA

NAM.	ENEO HUSIKA	WILAYA
1.	Mbuzini, Kijichi, Chuini, Mwera, Mtoni Sharifumsa, Dole, Mfenesini, Bububu Melinane	MAGHARIBI ‘A’
2.	Nyamanzi, Mazizini, Chukwani, Kiembe Samaki, Fuoni, Bweleo na Shakani	MAGHARIBI ‘B’
3.	Bwejuu	KUSINI
4.	Tunguu na Ndijani	KATI
5.	Nungwi, Pwani Mchangani, Banda kuu na Matemwe	KASKAZINI ‘A’
6.	Kitope	KASKAZINI ‘B’
7.	Baghani Shangani, Magomeni, Chumbuni, Jang’ombe na Saateni	MJINI

KIAMBATISHO F2:

MASHAURI MAPYA YALIYOPOKELEWA, YANAYOENDELEA MAHAKAMANI PAMOJA NA YALIYOTELEWA UAMUZI KWA KIPINDI CHA KUTOKA JULAI 2022 HADI MACHI, 2023.

MKOA HUSIKA		MASHAURI MAPYA ZILOFUNGULIWA	MASHAURI YALIYOOTOLEWA MAAMUZI	MASHAURI YANAYOOENDELEA MAHAKAMANI (MAPYA NA ZAMANI)
UNGUJA	Mjini Magharibi	49	48	68
	Kaskazini Unguja	30	28	34
	Kusini Unguja	21	20	35
PEMBA	Kaskazini Pemba	25	26	18
	Kusini Pemba	40	38	38
JUMLA KUU		**165**	**160**	**193**